**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| MHE. ZUBEIR ALI MAULID | - | SPIKA |
| 1. Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake |
| 2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani |
| 3. Mhe. Shehe Hamad Mattar | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda |
| 5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu |
| 7. Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi |
| 8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge |
| 10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | - | MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 11. Mhe. Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Nafasi za Wanawake |
| 12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali | - | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume | - | MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. Rashid Ali Juma | - | MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani |
| 15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais |
| 16. Mhe. Maudline Cyrus Castico | - | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais |
| 17. Mhe. Salama Aboud Talib | - | MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake |
| 18. Mhe. Juma Ali Khatib | - | MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais |
| 19. Mhe. Said Soud Said | - | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais |
| 20. Mhe. Khamis Juma Mwalim | - | Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe |
| 21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera |
| 22. Mhe. Shamata Shaame Khamis | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni |
| 23. Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete |
| 24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri | - | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani |
| 25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi |
| 26. Mhe. Chum Kombo Khamis | - | Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake |

| | | |
|---|---|---|
| 27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake |
| 28. Mhe. Lulu Msham Abdalla | - | Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake |
| 29. Mhe. Juma Makungu Juma | - | Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini |
| 30. Mhe. Abdalla Ali Kombo | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 32. Mhe. Ali Khamis Bakar | - | Jimbo la Tumbe |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji | - | Jimbo la Kwahani |
| 34. Mhe. Ali Suleiman Ali | - | Jimbo la Kijitoupele |
| 35. Mhe. Ame Haji Ali | - | Jimbo la Nungwi |
| 33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Nafasi za Wanawake |
| 37. Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Kiwengwa |
| 38. Mhe. Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid | - | Jimbo la Wawi |
| 41. Mhe. Hamida Abdalla Issa | - | Nafasi za Wanawake |
| 42. Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Shaurimoyo |
| 43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 44. Mhe. Hidaya Ali Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | - | Jimbo la Mtoni |
| 46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub | - | Jimbo la Paje |
| 47. Mhe. Khadija Omar Kibano | - | Jimbo la Mtambwe |
| 48. Mhe. Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi | - | Jimbo la Mtopepo |
| 50. Mhe. Makame Said Juma | - | Jimbo la Kojani |
| 51. Mhe. Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud | - | Jimbo la Bububu |
| 53. Mhe. Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 55. Mhe. Mohamed Said Mohamed | - | Jimbo la Mpendae |
| 56. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali | - | Jimbo la Uzini |
| 57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | - | Jimbo la Bumbwini |
| 58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 59. Mhe. Mussa Ali Mussa | - | Jimbo la Ole |
| 60. Mhe. Mussa Foum Mussa | - | Jimbo la Kiwani |
| 61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini | - | Jimbo la Dimani |
| 64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy | - | Jimbo la Chaani |
| 65. Mhe. Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 66. Mhe. Omar Seif Abeid | - | Jimbo la Konde |
| 67. Mhe. Panya Ali Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 68. Mhe. Rashid Makame Shamsi | - | Jimbo la Magomeni |
| 69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafasi za Wanawake |
| 70. Mhe. Said Omar Said | - | Jimbo la Wingwi |
| 71. Mhe. Said Hassan Said | - | Mwanasheria Mkuu |
| 72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |
| 73. Mhe. Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |
| 74. Mhe. Shaib Said Ali | - | Jimbo la Chonga |
| 75. Mhe. Simai Mohammed Said | - | Jimbo la Tunguu |
| 76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya | - | Uteuzi wa Rais |
| 77. Mhe. Suleiman Makame Ali | - | Jimbo la Ziwani |
| 78. Mhe. Suleiman Sarahan Said | - | Jimbo la Chakechake |
| 79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi | - | Nafasi za Wanawake |
| 80. Mhe. Ussi Yahya Haji | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir | - | Nafasi za Wanawake |

| | | |
|---|---|---|
| 83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 84. Mhe. Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar | - | Nafasi za Wanawake |
| | | |
| Ndugu Raya Issa Msellem | - | Katibu wa Baraza la Wawakilishi |

**Kikao cha Sita - Tarehe 14 Disemba, 2017**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

**Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum):** Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. *(Makofi)*

**Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa):** Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka mezani hoja kuhusu kuweka miundombinu bora kwa watu wenye ulemavu katika majengo, barabara, makaazi na maeneo ya kupumzikia na maeneo mengine yanayohusiana na hayo. *(Makofi)*

**Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa):** Mhe. Mwenyekiti, kuweka mezani maombi ya wananchi wa Kisakasaka Zanzibar, kuhusu namna wanavyoweza kufaidika kutokana na machinjio ya wanyama yaliyopo kwenye maeneo yao. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 30**

**Tatizo la Nyumba ya Makaazi Katika Kituo cha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)**

**Mhe. Bahati Khamis Kombo -** Aliuliza:-

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi wanastahiki pongezi kwa juhudi zao kubwa wanazozichukua kwa kuwaletea maendeleo wananchi wake, pia kuwajali vijana na kuendelea kuwapa taaluma mbali mbali ili wasijiingize katika vitendo viovu. Vile vile, wengine kuwaweka katika vituo vya Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) lakini katika kituo cha JKU kilichopo kwa pweza wapo vijana ambao wanaendelea kupata mafunzo ya kilimo. Kituo hiki kimekuwa na tatizo la makaazi, nyumba wanayokaa imepasuka viambaza na ndani hairidhishi na pia sehemu ya choo inatatizo.

(a) Je, Mhe. Waziri ameshawahi kukitembelea kituo hiko.

(b) Kama tayari, ni lini jengo lile litafanyiwa matengenezo.

(c) Kwa kuwa hadhi ya Kambi ya JKU siyo ya kuridhisha, kuna mpango gani wa kuifanyia ukarabati ikiwemo majengo ya kambi hiyo ya kambi hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikao, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ hufanya ziara za mara kwa mara katika maeneo yote yaliyo chini ya usimamizi wa ofisi kwa lengo la kuangalia hali halisi ya utendaji kazi. Aidha, ziara katika Kambi ya JKU Kwapweza zimefanyika kwa nyakati tofauti kuangalia utekelezaji wa shughuli katika kiuto hicho, pamoja na kupata fursa kwa uongozi wa Ofisi kushiriki katika uzinduzi wa uvunaji wa mpunga katika Kambi hiyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka suala la majengo ya Idara Maalum katika vipaumbele vya serikali. Kambi ya JKU Kwapweza ni miongoni mwa kambi zilizozingatiwa katika vipaumbele hivyo. Katika kufikia azma hiyo, JKU imeanza kuweka msingi wa jengo la Ofisi ya kituo hicho, na kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ujenzi wa kituo utaendelea kupitia fedha za maendeleo katika kituo cha Kwapweza Kisiwani Pemba.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kupitia mradi huu wa kuimarisha majengo hadi ya Kambi hii inategemewa kuimarika kwa vile kituo hichi kitakuwa na majengo ya kisasa.

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, ni mara nyingi tu tunaambiwa kwamba vituo hivi vitaimarika, lakini ni karibuni tu nimekwenda pale na kuona jinsi vijana wetu ile nyumba hali halisi ilivyo. Lakini kama haitoshi hata kile choo kimepasuka na sehemu wanayopikia iko karibu na choo kile.

Je, ni lini choo kile kitafanyiwa matengenezo, ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba hali ya majengo katika makambi yetu ya JKU haiko vizuri kama ambavyho nimewezakueleza, na sio kwa kituo hicho tu.

Vile vile ni juhudi ambazo nimejibu. Juhudi mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa katika kuona hali hii iondoke ili wapiganaji wetu pamoja na vijana wetu waweze kupata majengo ambayo yanalingana na shughuli zao ambazo wanazifanya.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu choo kwamba ni lini kitafanyiwa ukarabati. Naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba juhudi tunazifanya kwa makusudi ili kuona kwamba tumeanza ujenzi wa msingi ili kusudi tujenge jengo jipya. Lile kwa kweli sasa hivi limepasukapasuka na mambo mengine, kwanza tunataka tuongeze nguvu huko. Lakini suala la choo nadhani

tulichukuwe na tulifanyie kazi kwa haraka iwezekanavyo ili wapiganaji wetu wapate sehemu ya kujisaidia. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama. Nimuulize Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu yake mazuri. Kwa kuwa kituo hiki cha Kwapweza ni kituo ambacho kwa kweli kina muda na kinatakiwa kiwe mstari wa mbele katika masuala kama haya. Lakini Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako nimekusikia ulikuwa ukizungumza kwamba, sasa hivi kuna msingi au *foundation* ambayo imeshajengwa na ulisema ni majengo ya kisasa.

(a) Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa niulize tu kwamba huu msingi ambao umejengwa kwa majengo ya kisasa. Je, mpaka sasa hivi umeshagharimu shilingi ngapi.

(b) Jengo hilo likimalizika litagharimu shilingi ngapi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba msingi ambao umeshaanza kujengwa hadi sasa hivi umeshagharimu shilingi milioni tatu, na *target* ni kwamba tumekusudia mpaka kukamilika kwa ujenzi huo Mhe. Mwenyekiti, tutumie wastani wa shilingi 85,000,000/- na ninatarajia kwamba shughuli hiyo itakamilika ndani ya kipindi cha miaka miwili.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Nilipokuwa nasikiliza majibu ya Mhe. Naibu Waziri hayaendani sambamba na ule uhalisia hasa wa kuzitengeneza hizi kambi.

(a) Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti hii ya mwaka 2017/2018 mlipanga kutengeneza makambi mangapi.
(b) Je, miongoni mwa hizo kambi na Kambi ya Upenja iko katika hali mbaya zaidi kuliko nyengine. Je, imo katika utaratibu wa kuitengeneza katika bajeti hii au haipo kabisa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, nimwambie tu Mhe. Mwakilishi kwamba majibu ambayo nimeyatoa ndio majibu ambayo yenye uhalisia.

Vile vile kuhusiana na kambi, kwanza Kambi ya Upenja kwamba ni miongoni mwa kambi ambazo ziko katika hali ambayo hairidhishi. Lakini wakati nilipokuwa nikimjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo. Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba hali ya majengo yetu kwa ujumla katika kambi zetu nyingi haziko vizuri, na ndio maana sasa serikali imeandaa mpango wa makusudi wa kuweza kutengeneza *fund* maalum ambayo itafanya ukarabati wa majengo mbali mbali katika makambi yetu, pamoja na maanga ya wapiganaji wetu katika kambi zetu zote Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kwa mpango wa mwaka huu miaka ambayo tunaendelea katika mpango huo mkuu wa serikali, tumeanza na kambi ya KMKM na vile vile tunaendelea na kambi za Mafunzo. Hii hatukuchukua kuwa majengo yote tunaweza kuyajenga kwa wakati mmoja, tunaendelea kujenga lakini mpango huu unaendelea. Ni imani yangu kwamba na naomba nimtowe Mhe. Mwakilishi wasi wasi kwamba na Kambi ya Upenja pale muda

utakapofika basi itakuwa nayo itaingia katika mpango huo, ndio lengo la serikali kuona kwamba kambi zote za wapiganaji wetu ziko vizuri ili kusudi na wao wafanye kazi kwa mujibu wa utaratibu na jinsi ambavyo mahitaji yao yanaruhusu. Mhe. Mwenyekiti, naomba nitowe majibu hayo.

**Nam. 91**

**Ukosefu wa Mavazi Kwa Wanafunzi wa JKU Wakati wa Mahafali**

**Mhe. Ali Khamis Bakari** - Aliuliza:-

Tumeshuhudia mahafali ya vijana wa JKU walivyohitimu mafunzo yaliyopatikana na wakiwa wamevaa sare nzuri za Jeshi hilo ili kuendana na sherehe yenyewe, na kwa kuwa fomu zile walizokuwa wamevaa walisaidiwa kutoka Bara ili kufanyia sherehe hizo.

(a) Je, ni sababu zipi hadi leo vikosi vyetu vya JKU kuwa hakuna mavazi maalum kwa vijana hao.

(b) Je, ni lini kutatolewa sare hizo kwa vijana wetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 91 lenye vipengele (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, JKT na JKU zina historia ya muda mrefu ya mashirikiano mema. Vyombo hivi vya usalama vimekuwa vikishirikiana kwenye maeneo mengi, kama vile mafunzo, sherehe na matamasha, uzalishaji mali, shughuli za mifugo, kilimo na viwanda vidogo vidogo. Kufanya sherehe za kufunga mafunzo ya vijana ilikuwa ni sehemu ya mashirikiano yaliyojengwa kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi. Sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 91 lenye vipengele (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba, si kweli kwamba vijana wa JKU hawana sare makhsusi ya kutumia katika mafunzo yao. Fomu za kutumia vijana hao zipo, ingawaje zinapatikana kwa uchache sana kwa sababu za ufinyu wa ukomo wa bajeti.

(b) Mhe. Mwenyekiti, sare za vijana hawa zitapatikana kwa wingi pale tu serikali itakapoanza kuingiza bajeti ya vifaa vya mafunzo. Kwa sasa serikali imekuwa ikiwapatia vijana hawa, posho ya chakula, sabuni na gharama za matibabu tu wanapokuwa makambini.

**Mhe. Ali Khamis Bakari:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibi yake mazuri ambayo amesema kuhusiana na hali halisi ilivyo. Lakini pamoja na hayo naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba upo umuhimu wa kuongeza hiyo bajeti kwa ajili ya vijana wetu ili kupata hizo sare, badala yake kukosa wale wengine wanapata na wengine hawapati. Je,

hatuoni kwamba upo umuhimu huo sasa wa kuongeza hiyo bajeti, ili vijana hawa waweze kuenea hizo *uniform* zote.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba umuhimu upo mkubwa wa kuona kwamba tufanye jitihada za makusudi, ili kuona kwamba hali hii tunaongeza ufanisi katika kuona kwamba tunaliondoa hili tatizo ambalo limekuwa likiwepo kwa muda.

Kwa hivyo, kwa ufupi tu niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba pale ambapo itakuja bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ watusaidie katika kuona kwamba tunapitisha, ili kusudi jambo hili liweze kutatuka na vijana wetu wapate kupata mafanikio kama vile ambavyo serikali imekuwa ikikusudia au ikiwa imepanga kwamba vijana hawa kuwaondolea tatizo hilo.

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa fursa tena ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Waziri, vijana wetu wa JKU ni vijana wachapakazi sana, kwa nini vijana hawa wasipatiwe mafunzo ya kuweza kushona sare hizi wao wenyewe ili kuondosha tatizo hili, ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli vijana wetu wa JKU wanapokuwepo katika makambi kule tumekuwa tukiwapatia taaluma mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, moja ikiwemo ufundi pale ambapo panahitajika na kuonekana kwamba hizo nyenzo ziko za kutosha. Kwa hivyo, hili jambo tunataka kulifanya kama ambavyo nimesema kuwa tunataka tuone kwamba tatizo hili linaondoka. Ushauri wake alioutoa ni ushauri mzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, bado niombe tu suala la kikwazo cha bajeti, naomba tusaidiane ili hili jambo lifanikiwe na hiyo ndio dhamira yetu ya kuwepo kule kwenye makambi kwamba waweze kujifunza mambo mbali mbali, ilikusudi wawe raia wema kama vile ambavyo inatakiwa hivyo.

Juhudi nyengine ya ziada Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tuna kiwanda ambacho mwisho wa siku tunataka kitakapomalizika kiweze kufanya kazi ambazo zinafanana na kama vile Mhe. Mwakilishi ambavyo ameshauri. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kama Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo alivyouliza swali la msingi. Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza kwa upande wangu nasikitika sana kusikia kwamba askari wetu wanagaiwa ama wanasaidiwa sare kutoka upande wa pili, wakati sisi tunapitisha bajeti kwa ajili ya kuwashughulikia vijana hawa. Swali langu liko hapa.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri katika bango kitita ambalo analipeleka ndani ya serikali, hawaelezei kwamba askari wetu wana uhaba wa *uniform*, ili kuweza kutengewa bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuziba hiyo aibu iliyotokea.

(b) Mhe. Mwenyekiti, tuna taarifa kwamba kuna baadhi ya askari huwa wanakatwa katika mishahara yao katika ununuzi wa hizi sare. Je, suala hili namuuliza Mhe. Naibu Waziri ni kweli na kama ni kweli je, kuna uhalali gani wa kumkata askari ndani ya mshahara wake wakati yeye analitumikia jeshi na ule mshahara umsaidie katika matumizi yake binafsi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti naomba kujibu Swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikitoa majibu sijasema kwamba vijana wetu hawa tunagaiwa sare. Hiyo naomba tuweke *Hansard* sawa kwamba hatugaiwi sare, isipokuwa nimesema kwamba JKU na JKT zimekuwa na urafiki wa muda mrefu ambao urafiki huu unaweza kupelekea wakati mwengine baadhi ya mambo kuweza ku-*shares* ambayo pia sipendi kuyataja hapa hadharani. Sasa kama mtu ni rafiki yako mnaweza kuishi kwa upendo kama vile ambavyo mnakuwa mnafanya. Lakini kiufupi naomba niondoshe hii kauli kwamba tunagaiwa hatugaiwi ila nimesema tunazo lakini hazitoshelezi, nimeshawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu watusaidie ili kuona kwamba jambo hili tuweze kuongeza wigo mpana zaidi kuongeza upatikanaji wa sare ili kusudi kama ni kuazima kama ni mambo mengine ili yasitokee lakini kiufupi hatugaiwi sare.

Kuhusu kwenye Bango Kitita kuhusiana na kwamba hatuweki kipaumbele tunaweka vipaumbele vingi mbali mbali kutokana na mahitaji tuliyokuwa nayo, lakini lazima tuseme inafika wakati bajeti zetu zinakuwa na ukomo wa bajeti. Sasa ndio maana kipindi kile tulikuwa tumejaribu kushauri Waheshimiwa Wajumbe mutusaidie katika huku kwenye vikosi kwa kuwa kuna mambo mengi ambayo yanahitaji ufanisi mkubwa ni vyema tuuondoe ukomo wa bajeti katika vikosi ili kusudi haya mambo mengine yote yaingie kuna mambo mengi kule yanafanyika. Kwa hivyo niwaombeni sana Waheshimiwa pia na Mhe. Hamza Hassan Juma atusaidie kwa sababu hiyo hali anaifahamu vizuri.

Lakini jengine kuhusu kukatwa mishahara kwa askari kwa ajili ya kuchangia *uniform*, naomba nitoe majibu tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba hili bado kwa upande wetu sisi bado hatuna taarifa juu ya jambo hili na kama kuna jambo ambalo hizo taarifa zipo mimi nimuombe tu baada ya kumaliza kutoa majibu, nimuombe Mhe. Mwakilishi tukae pamoja anisaidie ili namna gani tufuatilie tubaini kama hili jambo lina ukweli kwa kiasi gani ili na sisi tuweze kuchukua hatua.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa majibu ya ziada pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri, ninataka kusema kwamba suala la sare kwa vikosi vyote hivi karibuni Serikali imeshatoa Shilingi Milioni mia tano na thalathini kwa ajili ya ununuzi wa sare mpya kwa vikosi vyote.

**Nam. 19**

**Malipo ya Kiinua Mgongo kwa Wafanyakazi Waliostaafu**

**Mhe. Mussa Foum Mussa** – Aliuliza:

Katika Bajeti ya mwaka 2017/2018, Wizara ya Fedha na Mipango iliomba Tsh. 11.48 bilioni kwa ajili ya malipo ya Kiinua Mgongo kwa wafanyakazi waliostaafu kazi.

Je, ni wafanyakazi wangapi  mpaka sasa waliokwishalipwa.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango** – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam 19 lenye kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha huu tunaoendanao 2017/2018, Serikali imelipa mafao kwa maana ya kiinua mgongo kwa wastaafu 116 kwa jumla ya Tshs. 10.736 bilioni zimetumika kwa malipo hayo hii ni sawa na asilimia 93.5 ya bajeti iliyopangwa ya Shilingi Bilioni 11.48.  Wastaafu waliolipwa ni wale tu ambao taratibu za malipo yao zimekamilishwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mhe. Mussa Foum Mussa:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa kipindi kikubwa wafanyakazi wanaostaafu huwa wanakaa kwa muda mrefu sana bila ya kupata malipo yao ya kiinua mgongo na kwa kuwa Serikali imeshaanza kujitahidi ili kuwalipa.

Je, kwa hao waliobakia na kwa vile wamekaa kwa muda mkubwa ni lini na wao watalipwa malipo hayo.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifutavyo.

Kwanza si sahihi Mhe. Mwenyekiti, kwamba sasa hivi kuna wastaafu wanaostaafu wanakaa muda mrefu, kwa sababu utaratibu wetu ni kwamba madai wadai wanadai kwa wasiozidi miezi mitatu tokea wastaafu. Sasa wanaostahiki kulipwa wamelipwa hadi waliostaafu mwezi wa Agosti, 2017. Hivi sasa kwa mujibu tuliyonayo tuna wastaafu wapatoa 304 ambao hao ndio wanaodai madai yao hivi sasa na taratibu zinafanywa ili kuhakikisha nao wanapata haki zao.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza suala dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya shemeji yangu naomba kumuuliza suala dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri amesema kwamba katika kipindi hichi hakuna mfanyakazi ambaye amestaafu aliyekuwa hajapata kiinua mgongo, katika Jimbo langu la Ziwani Shehia ya Wesha kuna mfanyakazi aliyekuwa akifanya kazi katika Wizara ya Afya huu ni mwaka kiinua mgongo chake hajakipata hadi leo na cheki ilipelekwa lakini pesa haikuingia.

a) Je, ni sababu gani iliyopelekea mfanyakazi yule amelitumikia taifa hadi leo kwamba kiinua mgongo chake hajakipata.

b) Ni hatua gani za kisheria kali mtazichukua kuhakikisha kwamba pesa hii imepotelea wapi ili kuhakikisha kupata pesa yake na yule aliyepewa dhamana mumpe adhabu.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Narudia kusema kwamba waliostaafu hadi mwezi Agosti, 2017 hao wote wameshalipwa stahiki zao kwa maana ya viinua mgongo hadi Agost 2017, ambao wanadai ni wale wa Septemba, Oktoba na Novemba ambao idadi yao ni 304. Sasa kama yupo mtu ambaye ana mwaka mizima hajalipwa naomba Mhe. Suleiman tuwasiliane baada ya kikao hichi ili tuweze kujua wapi kimekwama kwamba hajapata malipo yake hadi sasa.

**Nam. 43**

**Kukwama Kwa Ujenzi wa Chuo cha Amali Daya Mtambwe**

**Mhe. Omar Seif Abeid** - Aliuliza:

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein katika ziara yake ya kutembelea eneo la ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Amali Daya Mtambwe, aliagiza shughuli za ujenzi wa kituo hicho uanze mara moja. Lakini hadi leo ujenzi wa kituo hicho haujaanza wala dalili za kuanza hazipo kwani Mkandarasi ameshahamisha vitu vyake pamoja na nondo zilizokuwepo.

(a) Je, ni lini hasa ujenzi wa kituo hicho utafanywa ukitilia maanani eneo hilo lilikuwa na Mikarafuu isiyopungua mia mbili ambayo iling'olewa kwa ajili kupata eneo la ujenzi.

(b) Kama haiwezekani kujengwa kwenye eneo hilo, kuna mipango gani mwengine wa kupata eneo mbadala la kukijenga kituo hicho katika shehia ya Mtambwe Kusini.

(c) Je, ni sababu gani inayosababisha kuing'oa mikarafuu iliyokuwepo na kukimbilia kuanza kujenga kabla ya kufanya "*soil testing*" ili kubaini athari zinazoweza kujitokeza kwenye majengo kutokana na uhalisia wa ardhi yenyewe.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanziabr na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya ziara katika eneo la ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Amali huko Daya, Mtambwe tarehe 3 Aprili 2017 na kukuta kazi za ujenzi zimesita kwa kipindi kirefu. Kusita kwa kazi za ujenzi zilitokana na tofauti kati ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi ambapo Mkandarasi alianza kazi za ujenzi wa misingi bila ya kupata ruhusa ya Mshauri Elekezi ambaye kwa wakati huo alikuwa hajafika nchini. Mshauri Elekezi alikosoa kazi iliyofanywa kwa madai ya kutofikia viwango vilivyokubaliwa kwa mujibu wa Mkataba wa Ujenzi. Tofauti hiyo ilisababisha kazi kusimama na Wizara kuchukua hatua ya kuishirikisha Bodi ya Wakandarasi ya Zanzibar katika kufikia muafaka.

(a) Ujenzi ulitarajiwa kuanza tarehe 29/10/2017 kwa kazi za upimaji wa maeneo ya ujenzi wa majengo ya utawala, madarasa na dakhalia. Hata hivyo, ujenzi umeshindwa kuanza tena kutokana na Mshauri Elekezi kutorodhika na aina ya mchanga unaopatikana katika shimo la mchanga la Serikali lilioko katika Wilaya ya Micheweni. Wizara imegundua kuwa Mhandisi Msimamizi wa ujenzi kutoka Kampuni ya *New Tech*, amekuwa akitowa visingizio mbali mbali vya kucheleweshaujenzi na hivyo kutokana na tabia yake hiyo, Wizara imeagiza Kampuni ya *New Tech Consulting Group* ya Sudan kumuondoa mara moja Mhandisi wake na kuwataka walete msimamizi ujenzi mwengine, jambo ambalo wamelikubali. Hivyo kazi za ujenzi hivi sasa zimesita hadi atakapokuja msimamizi ujenzi mwengine.

(b) Wizara haina mpango wa kutafuta eneo jengine kwa ujenzi wa Kituo cha Amali kwani inaamini eneo hilo linafaa.

(c) Kama niivyotangulia keleza eneo hilo linafaa kwa ujenzi na hivyo kazi ya kusadafisha eneo na kung'oa miti iliyokuwepo katika eneo hilo ikiwemo mikarafuu mikongwe 67 na miembe mikubwa mitatu ilikuwa sahihi kwa maandalizi ya ujenzi.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa fursa ya kumuuliza suali dogo la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri yenye maelezo ya kina lakini bado kulikuwa kuna kitu kilikuwa kinanitatiza, kwa kuwa mkandarasi imeelezwa kwamba alijenga bila ya idhini ya Mshauri Elekezi na kwa sababu kazi ile imesimama kwa muda mrefu sasa suali langu.

a) Nataka nijue kutokana na kusimama kwa kazi ile ambayo yule mkandarasi alianza kuijenga asiiendeleze Serikali imepata hasara kiasi gani pale iliyosababishwa na mkandarasi huyo.

b) Ni lini huyo Mshauri Elekezi kutoka Sudan atamleta huyo au watakamilisha huo utaratibu wao wa mahitaji yanayohitajika ili ule ujenzi uanze na wananchi watoto wetu wa Kizanzibari wapate huduma ya elimu inayotarajiwa kutoka pale.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kwa uhakika hasara tuliyopata mpaka sasa ni hasara ya muda (*time*), lakini hasara ya fedha hakuna hasara yoyote iliyopatikana na kwa sababu ujenzi huu utakapoanza utaendelea kujengwa kwa idadi ya fedha zile zile zilizokisiwa mwanzo kwa hivyo hakuna hasara ya kifedha.

b) Niseme kwamba Wizara tayari imeshawasiliana na Kampuni ya Kandarasi na wamekubali kumuhamisha, lakini bahati nzuri kwamba huyu *Consultant* aliyopo sasa anamaliza mkataba wake Januari hii. Kwa hivyo hapa patakuwa hakuna hasara ya kuvunja mkataba, atakuwa amemaliza muda wake kwa hivyo analeta mwengine, kwa hivyo atapoletwa mwengine baada ya Januari basi hapo kazi itaanza mara moja.

Lakini nataka niseme pia kwamba *Consultant* huyu amekuwa na tabu sana hata jana tulikuwa tunazungumza naye pamoja na *Mishen ya IDB* basi ameleta masharti mapya tafauti na aliyoyasema nyuma, jana alisema kwamba anahitaji michoro mipya. Sasa mtu kama huyu kweli hatuwezi kufanya naye kazi anabadilika kila siku.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe naomba sana naona minong'ono imezidi mno Mhe. Shehe Hamad Matar kwa suala la nyongeza.

**Mhe. Shehe Hamad Matar:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza suala la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara ya Elimu ilichagua vijana kutokana na yale maeneo ambako kuwa kunategemewa kujengwa Chuo hicho cha Mtambwe na kukubali kuwagharamia gharama za kujikimu, vijana hao walitoka sehemu mbali mbali za kisiwani kule Pemba wakaja haka kupata mafunzo hayo. Lakini vijana hawa wamekuwa wanapata matatizo mara kwa mara kuhusu maslahi.

Je, ni lini hadi leo Serikali imechukua utaratibu ambao kuwa hautokuwa na usumbufu kuweza kupata maslahi yao kwa wakati ambao kwa hivi sasa wanapata tabu wanachi hao kutoka sehemu mbali mbali za Mtambwe na kwengineko.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kuna wanafunzi tunawafundisha na tunawalipia katika mfumo wa masomo ya Vyuo vya Amali, fedha za kuwalipa zipo isipokuwa kulikuwa na hitilafu kidogo za utendaji na suala hilo linafanyiwa kazi na wakati wowote baada ya kumaliza watalipwa mafao yao.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri.

Lakini Mhe. Waziri katika majibu yake alisema kwamba kutokana na jengo liliposimama anategemea gharama itakuwa ni ile ile ambayo itajengewa jengo lile.

a) Je. Waziri anatuthibitishia vipi kama gharama hizo hazitoongezeka kwa sababu mkandarasi yule anaweza akashindwa na akataka mkandarasi mwengine na gharama zikazidi, je gharama hizo atabeba nani.

b) Imeonekana katika majengo mengi hata Wizara ya Elimu ni kwamba baada ya kumaliza mkataba majengo yale yanaleta matatizo na halafu inakuwa kisheria ya Mkataba ule umemalizika.

   Je, Waziri katika majengo mapya ambayo anajengesha sasa hivi Mkataba wake kuna dhamana maalum anayozuia kwa yule Mkandarasi mpaka anapomaliza mkataba wake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Ni kweli yanaweza kutokea mabadiliko ya kupanda na kushuka kwa gharama za vifaa vya ujenzi, lakini hili limezingatiwa tokea mwanzo katika gharama za ujenzi, kwa hivyo hatutarajii kwamba kutakuwa na ongezeko lolote. Lakini endapo litatokea basi hatua nyengine zitachukuliwa zaidi ili kuona kwamba majengo haya yanakamilika na yanajengwa ipasavyo.

Kuhusu mikataba na wajenzi wapya tuliowapa kazi bado suala la muda tunalizingatia, muda *guarantee* upo, lakini tunakwenda mbali zaidi sasa tunajaribu kufuatilia tokea awali na niseme kwamba tokea michoro tumeifuatilia kwa pamoja kwa kusaidiwa na ma-*engineers*, tukafanya vikao vya ma-*engineers* ili kuona kama michoro yenyewe iko safi au haiko safi, katika hatua za ujenzi kunakuwa na *Resident Engineers* na wetu Wizara ya Elimu wapo ili ku-*control* ubora. Kwa hivyo tunatarajia kwamba majengo ambayo yatajengwa sasa yatakuwa na ubora unaotakiwa ahsante sana.

**Nam. 78**

**Ukosefu wa Ajira Kwa Vijana Wanaojitolea Waliomaliza Masomo Yao Bila ya Kuajiriwa**

**Mhe. Omar Seif Abeid** - Aliuliza:

Kwa kuwa kuna wafanyazi ambao wanajitolea kwa muda mrefu zaidi ya miaka 3 katika skuli mbalimbali za Unguja na Pemba, na kwa sababu Serikali imekuwa ikitoa kipaumbele kwa walimu hasa wa sayansi na kwa sababu katika skuli za Jimbo la Konde wapo vijana kama hao wanaojitolea ambao ni walimu wa sayansi na wana elimu ya Kidato cha Sita *"form six"* kwa muda wa miaka (4) na hadi leo hawajaajiriwa jambo ambalo linasikitisha sana pamoja na kwamba Serikali imeshatoa ajira kwa walimu.

(a) Je, ni lini Serikali itawaajiri vijana hao ambao wameonesha moyo mkubwa wa kujitolea kwa nchi yao.

(b) Je Wizara ina mpango wa kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana walioonesha uzalendo badala ya kuwaajiri wale ambao baada kumaliza tu kusoma wamekaa wakisubiri kuajiriwa na kuachwa hawa wanaojitolea.

(c) Je, Wizara haioni kwamba kuanzisha mpango huu wa kuwaajiri vijana ambao wapo tayari wameshajitolea kutatusaidia hata kupunguza tatizo la walimu maskulini ukitilia manani kwamba vijana wanaomaliza chuoni ni wengi wanaosubiri ajira.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Wizara inakiri kuwa katika kipindi cha nyuma baadhi ya skuli za Serikali zimekuwa na tabia ya kuwatumia vijana wa kujtolea kusomesha katika skuli. Utaratibu huu ulifutwa kwa barua rasmi ya Wizara walioandikiwa Walimu Wakuu wa skuli zote kutokana na kukiuka taratibu za Serikali za uajiri. Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014, Kanuni ya 138 inakataza wafanyakazi wa kujitolea na naomba ninukuu, "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi hatoruhusika kuweka wafanyakazi wa kujitolea katika Taasisi yake", mwisho wa kunukuu.

Pia, napenda kufahamisha kuwa Serikali haina utaratibu wa kuajiri walimu ambao hawajasomea mafunzo ya ualimu. Nina washauri vijana waliomaliza masomo ya Kidato cha Sita na wanaendelea kujitolea katika skuli zetu licha ya Wizara kukataza kujitolea na wanaipenda kazi ya ualimu waache mara moja na waombe kujiunga na masomo ya Stashahada au Shahada ya Ualimu kama walivyofanya wengine na watakapohitimu watatambuliwa rasmi kuwa walimu. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo:

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Tume ya Utumishi Serikalini inaajiri wafanyakazi mbali mbali wa sekta ya umma na walimu kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011, Kifungu cha 57 pamoja na Kanuni yake ya mwaka 2014, Kanuni ya 7(i) - 7(v) ambayo inatoa fursa sawa kwa waombaji wote wenye sifa kwa kuzingatia vigezo, masharti na sifa zinazotangazwa na Tume ya Utumishi Serikalini. Sheria na Kanuni za Utumishi kuhusu ajira haitoi upendeleo wowote kwa walimu au wafanyakazi wanaojitolea katika ajira.

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina utaratibu wa kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana wanaojitolea kama nilivyotangulia kusema ingawa uzoefu walio nao unaweza kuwasaidi katika kufikiriwa maombi yao. Utaratibu uliopo unahusisha waombaji wote wenye sifa za nafasi za kazi zinazotangazwa bila kubagua kundi fulani.

(c) Walimu wanaojitolea wana fursa sawa ya kuomba ajira ya kazi ya ualimu pale nafasi za kazi zinapotangazwa kama watakuwa na sifa zinazotakiwa. Kujitolea kwao kufundisha kunaweza kuwajengea sifa za uwezo na uzalendo lakini sio kigezo kinachotambulika katika uajiri. Ahsante.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri yenye ufafanuzi ya kina kanukuu vipengele vya Kanuni ya Utumishi wa Umma hatuvipingi ni utaratibu wa kisheria ambao tumeuweka. Lakini pia sheria inawakataza vijana wasijitolee, ni sawa na sisi maskulini mwetu tuna upungufu mkubwa wa walimu na agizo ni kwamba watu wasijitolee.

a) Mimi ningependa kujua. Je, ni idadi gani ya walimu wanaohitajika ili kukidhi mapengo katika maskulini mwetu, hasa wale wa masomo ya sanyansi ambao ndio kilio kikubwa
.
b) Je, ni vijana wangapi waliomaliza ngazi ya Stashahada kwa mwaka wa masomo 2015, 2016, na 2017 ambao hadi leo hawajapatiwa ajira kwenye hiyo fani ya sayansi. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa suala hili linahitaji takwimu na utafiti zaidi, kwa hivyo naomba nimjibu kwa maandishi hapo baadae. Ahsante.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini pia nimuulize suali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa vijana wetu hawa ambao wanajitolea wanaonyesha moyo wa uzalendo katika nchi yao. Na katika Wizara yetu tunatatizo la walimu kila wakati mpaka muda huu tunaousema tuna matatizo ya walimu.

(a) Je, serikali haioni kufunga mikataba na vijana hawa ambao wanajitolea ili pale shida zinapotukuta ili tuweze kuendelea nao. Kwa sababu kuendelea kuwaacha vijana hawa ambao wao kwa moyo wao wa kizalendo hatuwalipi moyo wa kizalendo ndiyo wameonyesha sura hii.

(b) Je, kuna walimu tangu 2007 ambao wameshasomea na hawajaajiriwa mpaka hii leo. Serikali haioni kuwachukua wakati wa uwajiri kuzingatia pia wale walimu waliosomea kwa muda mrefu ambao hawajapata ajira ili wakaweza kuajiriwa na wao tukizingatia kile walichokisoma kinaweza kikapotea.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo.

(a) Kwa sababu Wizara ya Elimu haina mpango wa kufunga mkataba katika suala hili la walimu wanaojitolea. Lakini itakapofika hatua tukaona kwamba ipo haja ya kufanya hivyo tutafanya, lakini kwa sasa hakuna haja hasa ukitilia maanani kwamba sasa hivi serikali imetupa kibali cha kuajiri walimu wengi kidogo. Kwa hivyo tunatarajia suala hili la upungufu wa elimu litaendelea kutatuka hatua kwa hatua.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ajira kwa mujibu wa labda tuseme kwa *seniority* ya waliotangulia kumaliza masomo, pia hakuna utaratibu huo kwamba inatokezea fursa ya ajira serikali kupitia Tume ya Utumishi inaitangaza kwa mujibu wa sifa zinazotakiwa za ajira hiyo wala sio kwa mujibu nani amemaliza mwanzo au amemaliza mwishoni. Lakini hata hivyo kwa kuwa suala hili au kwa kuwa jamo hilo ni ushauri tunaweza tukalifikiria ili kuwafanya na wao hawa waliotangulia wasisahau yale waliyojifunza, lakini kwa sasa hatulazimiki kufanya hivyo. Ahsante sana.

**Nam. 75**

**Malipo ya Miti ya Mazao IIiyoathiriwa na Shughuli za Maendeleo**

**Mhe. Omar Seif Abeid -** Aliuliza:

Kwa kuwa Wizara ya Kilimo ndio yenye jukumu la kutathmini miti yote ya mazao ya kilimo cha chakula na biashara inayolipwa kutokana na kuathiriwa na shughuli mbali za maendeleo kama vile sehemu za uwekezaji, ujenzi wa barabara, kazi za kusambaza umeme, na sababu bado inaonekana kwamba bei inayolipwa kwa waathirika hao ni ndogo kutokana na uhalisia wenyewe wa kupanda bei ya mazao yanayovunwa kwenye miti hiyo.

(a) Je, serikali inalipa kiasi gani kwa shina la mkarafuu, muembe, mnazi au mchungwa inayozaa vizuri.

(b) Je, kuna mpango gani wa kufanya marekebisho ya bei za kulipa fidia kwa miti ya Mazao ya Biashara.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 75 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na hoja ya Mheshimwa Mwakilishi kwamba Wizara ndio inayohusika na tathmini ya miti yote ya mazao ya kilimo, chakula na biashara inayolipwa kutokana na kuathiriwa na shughuli za maendeleo hapa nchini. Kwa mujibu wa Kanuni L.N 79 ya 2013 ya bei na fidia kwa mazao ya chakula na miti, hivi sasa shina moja la Mkarafuu unaozaa vizuri linalipwa Shs.300,000/-, Muembe Shs.250,000/-, Mnazi Shs.150,000/- na Mchungwa Shs.75,000/-.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeunda Kanuni ya mwaka 2013 na mwaka 2014 ambayo inatoa muongozo juu ya fidia inayotakiwa kulipwa kulingana na hali ya miti au mazao inayoathirika. Hata hivyo Wizara baada ya kupata ushauri kwa wadau imetayarisha mapendekezo ya fidia mpya na kuyawasilisha Wizara ya Fedha kwa ajili ya utekelezaji kwa mujibu wa sheria. Aidha, bei mpya za fidia kwa sasa ni shina la mkarafuu unaozaa vizuri litalipwa shilingi 400,000, muembe Shs.350,000, Mnazi Shs.300,000 na Mchungwa Shs.100,000.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri yenye ufasaha na yenye muelekeo kwa wakulima wetu, lakini napenda niulize suali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa thamani inayolipwa hadi sasa ya miti hiyo kama tulivyosema na wewe ukakiri kwamba imeshapitwa na wakati. Sitoamini kama imepitwa na wakati. Kutokana na kupanda bei kwa mazao yanayotokana na miti hiyo kama vile mchungwa, tulivyoieleza miembe, mikarafuu na kadhalika. Na kwa sababu kuna ujenzi wa barabara zinazojengwa hivi sasa mfano wa Bububu/Mahonda/Mkokotoni, Fuoni/Kombeni zinazotarajiwa kujengwa, Kongwe/ChakeChake/Wete ambayo ina miti mingi inayobidi ilipiwe fidia.

(a) Je, Serikali Wizara haioni hivi sasa kuwalipa fidia hii iliyopo hivi sasa wananchi wetu, wakulima wetu tutakuwa tunawaumiza.

(b) Haoni kwamba bei zinazolipwa kwa sasa hazifiki hata nusu ni sawa na bei za kukodisha mfano kumlipa shina la mkarafuu shilingi laki tatu au muembe shilingi laki tatu unusu, huoni ni sawa sawa na bei ya kodisha wakati mti ule tumeuwondoa. Lini tutazibadilisha hizi bei ili wakulima wetu waweze kufaidika. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Konde suala lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwakilishi hizi bei nilizokutajia zilikuwa ni za zamani na nyengine nimekutajia bei mpya. Lakini vile vile kama unahisi hazitoshi basi tunaweza tukakaa sisi na wale watu wa tathmini ili baadaye tujue ni bei gani. Ahsante sana.

**Mhe. Asha Abdalla Mussa:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ili niweze kuuliza suali la nyongeza.

Mhe. Waziri katika jibu lake mama amesema kwamba kila mti kisheria una bei yake. Lakini kuna wananchi wa Shehia ya Pangeni/Kilombero na Mchangani ambao walikuwa wanalima katika bonde la Mtomzigua, lakini bonde hilo amepewa Muwekezaji wa Kiwanda cha Sukari kwa ajili ya kulima miwa kwa ajili ya kiwanda hicho. Lakini kabla ya wananchi hao kulipwa fidia muwekezaji huyo ameweza kuvuruga vipando vya wananchi hao.

(a) Je, Wizara yako itawasaidia vipi wananchi hao waweze kulipwa haki yao kisheria.
(b) Je, ni lini watapewa fidia zao hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi jibu lake kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwakilishi ningeomba utusaidie watu hao ambao wamechukuliwa vipando vyao vimekatwa wangekuja ofisini tukaa tukaongeza tukajua ni jinsi gani mazao yao yalivyokuwa na kila kitu. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana swali litaulizwa tena kwa Wizara hiyo na Mhe. Omar Seif Abeid.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa sababu suali kama hili lilipatiwa majibu ya kina juzi na niliridhika nayo naomba kuliondoa suali hilo.

**Nam. 113**

**Juhudi za Serikali za Kujenga Viwanda Pemba**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said -** Aliuliza:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika juhudi zake za kuleta maendeleo kwa wananchi wake, lakini kwa upande wa Pemba bado kunahitajika viwanda vikubwa na vidogo kwa maendeleo ya nchi yetu. Takriban kisiwa cha Pemba kina matunda ya aina nyingi na mazao mbali mbali kwa uhalisia wake, lakini mpaka sasa bado hakina viwanda vya matunda kwa ajili ya kutengeneza " *juice*" na mazao ya chakula kwa ajili ya kuuza katika nchi za nje. Kutokana na tatizo hilo sijaona harakati za serikali zilizotayari au za watu binafsi katika kuwekeza katika viwanda.

(a) Je, serikali haioni umuhimu wa haraka kuchukuwa jitihada za kujenga viwanda vya kusindika chakula na "juice" kwa kuokoa mazao ambao yanapotea kwa msimu kwa sababu hayawezi kustahamili muda mrefu.
(b) Ni mpango gani wa haraka uliowekwa na serikali ili kuendana na kasi ya kujenga viwanda vidogo vidogo katika kisiwa cha Pemba, kwa ajili ya kuokoa mazao hayo kwani inaonesha sekta binafsi haijakuwa tayari na mpango huo.

(c) Je, serikali haioni kuwa ni hasara kupoteza mazao hayo kibiashara, kilimo na fedha za ndani na kigeni.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko -** Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 113 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, katika miaka ya karibuni kumekuwa na muamko mkubwa wa wananchi wa Unguja na Pemba katika kuzalisha bidhaa nyingi za kilimo ambazo wakati wa kilele cha misimu ya uvunaji wake hupelekea kushuka sana bei au hata kuharibika kwa sehemu kubwa ya mazao hayo. Suluhisho la kudumu kwa matatizo hayo ni kuwa na viwanda vya kusarifu mazao hayo.

Hata hivyo inafaa ikumbukwe kuwa serikali kwa makusudi na kwa nia njema kabisa iliamua kujiondoa katika shughuli za kuendesha biashara na viwanda tangu mwaka 1986 na kuiwachia sekta binafsi kuendesha shughuli hizo. Ili kufanikisha azma hiyo, serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kuboresha na kurahisisha uwezezaji wa viwanda ikiwa ni pamoja na kuweka vivutio vizuri chini ya Mamlaka ya Uwekezaji (*ZIPA*) na kufanyiwa mapaitio Sera ya Viwanda ya mwaka 1998.

Serikali itaendelea kuchukua hatua hizo za kuboresha mazingira ya uwekezaji pamoja na kuwahamasisha zaidi wawekezaji kwenye sekta ya viwanda.

Kwa upande mwengine viwango vya uzalishaji wa matunda na mazao mengine ya kilimo (ukiwacha mwani) bado havitoshelezi mahitaji ya kiwanda kufanya kazi kwa kipindi kirefu cha mwaka na kuleta faida kwa mwekezaji. Kwa mantiki hiyo, inafaa wananchi waongeze uzalishaji wa bidhaa ili wawekezaji washawishike kuanzisha viwanda vya kusarifu bidhaa hizo.

(b)Katika hatua ya kuendana na kasi ya kujenga viwanda vidogo vidogo katika kisiwa cha Pemba na Unguja, kwa ajili ya kuokoa mazao ya kilimo na kuzalisha bidhaa nyengine za aina mbali mbali. Serikali inapendekeza kuunda Wakala wa kusimamia maendeleo, kuratibu na kutoa misaada kwa miradi yote midogo midogo na ya kati ya viwanda vya wajasiriamali. Wakala huyo atajuliana kama "Wakala wa kuendeleza viwanda vidogo vidogo na vya kati" (*Small and Medium Industrial Development Agency - SMIDA*).

(c) Serikali inatambua hasara kubwa inayopatikana kutoka na kuharibi kwa matunda, na ndio maana inashajihisha usarifu wa mazao hayo, ama kupitia viwanda vya mtu mmoja mmoja au vikundi vya ushirika vya wajasiriamali na wawekezaji wa nchi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na namshukuru saa Mhe. Waziri katika majibu yake mazuri na yenye ufafanuzi mzuri. Lakini kabla ya hapo kwanza napenda niseme kwanza nimsifie kwa Wizara yake pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kupandisha zao la karafuu bei ambayo ya uhakika ambayo tunafaidika nayo sana.

Namuuliza Mhe. Waziri kwamba kule Pemba katika jitihada za Mhe. Rais za kukuza zao la karafuu katika bei kubwa imefanyika baadhi ya wakulima wana uwezo katika msimu kupata kuanzia milioni 50 mpaka milioni 100 kutokana na msimu, lakini pesa

zile nyengine zinaishia kwenye mambo ya kununua magari na kujenga vitu vyengine kwa sababu hawana utaalamu wa viwanda.

(a) Je, serikali katika kuwasaidia wananchi wale imeshafanya *research* ya kujua kama viwada cha matunda vidogo vinagharimu shilingi ngapi ili wale wakulima wakubwa wangewaendea na kuwaelekeza kwamba ikiwa na kiwanda hichi unaweza ukazalisha biashara hizo. Ningeomba Mhe. Waziri amefanya jitihada gani katika kuwaendea wale wakulima wakubwa na wao waweze kuanzisha viwanda kwa sababu hawajajua kusafiri na kwenda kutafuta mashine hizo,

(b) Kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba masuala haya wamewekekewa wawekezaji katika viwada hivi, lakini kama wawekezaji hao hawajaja. Je, serikali haioni umuhimu wa ku *take off* katika sekta hii ya biashara kwa ajili ya kuokoa mazao hayo.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibu suala la nyongeza la Mheshimiwa Mwakilishi kwamba kweli bei ya karafuu ni nzuri sana na imetia hamu wananchi wengi wa Pemba kusimamia zao la karafuu na wanapata faida kubwa.

Na sisi kama Wizara yetu ya Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha hata Tume ya Mipango tumefanya utafiti kuona kwa kiasi gani hizi fedha zinapatikana katika karafuu zinatumika. Nakubaliana naye kwamba pesa zinazotoka kwenye zao la karafuu bado hazijaweza kutumiwa kwa ajili ya uwekezaji hasa katika sekta hii ya viwanda au sekta ya biashara. Fedha nyingi ambazo zimetoka katika Sekta ya Karafuu mara nyingi tumezikuta hazipo katika mabenki yetu zinapelekwa Mabenki ya Nje, kama Tanga, Dar-es-Salaam na kwengineko lakini zile zinazobakia ndani ya Pemba zinakuwa zinatumiwa kwa ajili ya mambo madogo madogo ya kujenga nyumba na mambo mengine kama hivyo wanaona wenyewe wana familia muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa sababu suala hili tumeliona tunalifanyia kazi sasa hivi, lakini vile vile niombe niseme tu kwamba kwa kuwa tumeanzisha huu Wakala wa Viwanda Vidogo Vidogo, moja ya kazi yao ni kukaa kuwatayarishia wanaita utafiti wa kitaalamu na vile vile taratibu nzima ya kufanya biashara na kuanzisha viwanda na kufanya biashara na masoko. Kwa hivyo mpaka hapo tutakapoanza kazi hiyo kwa sababu hivi hatujakuwa na Idara hiyo ndani ya Wizara yetu lakini ndiyo tumeshaiweka kitakapoanza kitengo hichi tutaanza shughuli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba niseme tu kwamba katika utaratibu huo wa *SMIDA* tunataka mjasiriamali mdogo mdogo na wa kati aweze kuanza mambo yake kwa ukamilifu na kwa utafiti na kwa utaalamu wa hali ya juu. Ndio maana tukasema hata zile gharama za kununulia vifaa kwa mfano mashine, tutachukua *guarantee* sisi kama serikali ili aweze kupata mashine zinazokwenda na wakati. Huku nyuma tulikuwa kazi hii hatujaanza kuifanya kwa sababu chombo hiki kilikuwa hakipo.

Niseme kwamba kule Pemba wapo wajasiriamali wazuri tu na wanafanya kazi, pia wamepata utaalamu wa kuweza kufanya biashara zao. Lakini bado utaalamu waliokuwa nao kama nilivyosema pale mwanzo uzalishaji wa mazao haya ya kilimo kule Pemba na Unguja pia bado haujakdhi kuwa na viwanda, kinachofanyika kwa muda mfupi ni kuwa na viwanda vile

ambavyo vitakavyokidhi mahitaji ya ndani yakiwemo wananchi wenyewe na vile vile katika Sekta ya Utalii na Sekta ya Usafiri.

Kuhusu suala la pili Mhe. Naibu Spika, ningeomba nirudie suala hilo.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Kwanza nikushukuru sana kwa jibu lako hilo la kwanza umelijibu vizuri sana lakini swali la pili nilikuwa nakuuliza mheshimiwa ni kwamba kwa sababu tumetoa nafasi kwa wawekezaji na kutoka mwaka 1998 tumefuta hiyo mambo ya uwekezaji kuwa katika Serikali. Sasa lakini tumeona kwamba nafasi tuliyoitoa wawekezaji hawajaitumia hatuoni kwamba kuna haja ya Serikali kuchukua nafasi hiyo kwa kulinda mazao haya.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mhe. Suleiman kama hivi ifuatavyo.

Pamoja na kwamba Serikali imejitoa katika suala zima la kuanzisha viwanda na biashara lakini bado inayo nafasi kuangalia katika maeneo ambayo ni muhimu kuweza kufanya kazi. Kwa mfano suala la Shirika letu la *ZSTC*, Kiwanda cha Makonyo kile ni kiwanda ambacho mia juu ya mia ni cha Serikali. Hivyo pindipo Serikali ikiona kama kuna haja kimkakati kuweka viwanda ambavyo vinahusiana na kusaidia mazao wananchi na vile vile kupata tija kubwa sana kama mazao yale tunatakiwa tuyauze nje haitosita kufanya hivyo.

Kuna njia mbili Mhe. Mwenyekiti, njia ya kwanza kuwa na wabia wenzetu wa nje ama wa ndani kufanya ubia na sisi tukachukua *share* katika viwanda vile lakini ya pili Mhe. Mwenyekiti vile vile kuna vyombo vyetu hapa mashirika yetu, kwa mfano mabenki na vyombo vyengine vya fedha tunaweza nayo kushirikiana na wawekezaji wa ndani na wa nje kuweza kuweka viwanda vile ambavyo tunaviona muhimu.

Sasa hivi tuko katika hatua ya pili Mhe. Mwenyekiti, nayo ni kufanya *research* wanafanya utafiti yakinifu wa kuangalia hali ya viwanda na hali ya uzalishaji wa ndani, tukishamaliza kazi hiyo tutaweza kujua sasa tunafanya nini kama Serikali ili kuwahami wakulima wetu. Ni kweli tunajua kwa mfano watu wanaolima tungule kipindi cha mwaka huu walipata hasara tunajua wanaolima matikiti wanapata hasara yote haya tutakuwa tunachukulia kipau umbele katika utaratibu wa bajeti ya 2018/2019.

**Nam. 87**

**Uanzishwaji Viwanda wwa Ajili ya Mafunzo kwa Vijana**

**Mhe. Ali Khamis Bakari -** Aliuliza**:**

Kwa kuwa Serikali zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinasisitiza na kuimarisha zaidi suala la viwanda, na kwa kuwa Tanzania Bara kumeanzishwa viwanda vya JKT Suma ili kutoa mafunzo na ajira kwa vijana.

a) Je, ni sababu zipi hadi leo Zanzibar ikawa haijaanzisha Suma JKU.
b) Je, ni lini Serikali itaanzisha viwanda katika Makambi yetu ya JKU.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Aki Khamis Bakari Mwakilishi wa Tumbe lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ili kupata taarifa kwa kina juu ya suala hili lingefaa zaidi lijibiwe na katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa sababu hili jambo linahusu Vikosi vya SMZ lakini kwa kuwa linahusiana na masuala ya viwanda, naomba nieleze yafuatayo:-

JKT na JKU ni taasisi mbili tofauti zilizo katika pande mbili za Jamhuri ya Muungano, ingawa taasisi hizi zina mashirikiano makubwa ya karibu sana baina yao. Ni kweli kwamba hapa kwetu hatuna SUMA JKU, lakini naomba kumuarifu Mhe. Mwakilishi kwamba vikosi vyetu vya Idara Maalum za SMZ, ikiwemo JKU, KMKM, Valantia na Vyuo vya Mafunzo, vinaendeleza pia miradi ya viwanda mbali mbali na shughuli zao za kawaida.

Ushahidi wa hayo, Mhe. Mwenyekiti, ni Kampuni ya *Zanzibar Quality Tailoring* ya ushoni iliyopo *Amaan Industrial Park*, ambayo inamilikiwa kwa pamoja na vikosi hivyo vya Idara Maalum. Vile vile baadhi ya vikosi hivyo vinaendesha miradi mengine kama ya useremala na kilimo.

Bila shaka Mhe. Mwenyekiti, vikosi vyetu vitaendelea kushiriki katika uzalishaji wa viwanda, kama dalili zilivyoanza kujitokeza kwa kikosi cha Valantia kuanzisha Kiwanda cha Viatu.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Khamis Bakari:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Waziri wangu mama yangu Balozi Amina kwa majibu yake mazuri kweli suala hili lilikuwa limehusiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi, lakini pamoja na majibu yake mazuri naomba nimuulize swali la nyongeza.

Je, hatuoni upo umuhimu sasa wa JKU kuwepo kwa viwanda hivi ili vijana wanaokwenda kujiunga pale na kupata taaluma baada ya kumaliza ili waweze kujiajiri wenyewe.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:**Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba uko muhimu wa kuongeza viwanda kama hivi kwa sababu tayari wameshaanza viwanda vya ushoni na sasa hivi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshawapa fedha kwa ajili ya kiwanda cha kutengeza viatu. Lakini kama ninavyoelewa kwa kukaa na Mhe. Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa na Vikosi kama uko utaratibu mkubwa zaidi wa kuongeza maeneo zaidi ya viwanda kwa ajili ya kuweza kuwafanya vijana wetu hawa wakaweza kupata ile taaluma na utaalamu wa kuweza kuendelea na shughuli zao wanapotoka.

Mhe. Mwenyekiti, binafsi wakati tunazungumzia suala zima la kuanza kuwa na chuo cha kufundisha vijana wetu ushoni wa kitaalamu na ushoni wa kisasa tulikubaliana na Wizara hii na Waziri anayehusika kwamba iko haja kile Chuo chao ambacho sasa hivi wataondoka pale viwanda vidogo vidogo tukabidhiwe Wizara ya Biashara na Viwanda, ili tuweze kuongeza na kuweka Chuo kikubwa zaidi cha kuwafundisha vijana wote wa Zanzibar ushoni wa kitaalamu kwa sekta ya utalii. Kwa hivyo kama nilivyosema kuna umuhimu huo na Serikali pia imeshaanza kazi hii kushughulikia na wizara inayohusika imeshapewa fedha za kiasi za kuziendeleza shughuli hizi za mambo ya viwanda ndani ya vikosi vyetu.

## MUONGOZO

**Mhe. Simai Mohamed Said:**Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa wakati Mhe. Waziri anayehusika mwenye dhamana Biashara na Viwanda akitoa majibu kwenye swali namba 113 na mimi kwa upande wangu nilisimama nikisubiri maswali ya nyongeza, sasa nilikuwa nataka kujua tu kupata muongozo wako.

Je, ni utaratibu tayari umeanza rasmi kwamba sasa hivi maswali ya nyongeza yatakuwa hayapo au ulikuwa haujaniona..

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Simai utaratibu kama Kanuni inavyojileza maswali ya nyongeza yapo lakini kulingana na shughuli zetu na muda ndio maana nikawa natoa ruhusa kwa maswali mawili au moja kutokana na muda. Kwa hivyo nilikuona na natumai utapata nafasi nyengine kwa hiyo utauliza. Mhe. Simai tumemaliza naomba ukae tuendelee.

**Mhe. Simai Mohamed Said:** Usije ukanitoa tu.(*Kicheko*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Makame Suleiman nimekuona.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naitwa Suleiman Makame Ali. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya mama yangu Mhe. Balozi Amina Balozi wa heshima nampongeza sana kwa majibu mazuri lakini naomba kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifugu (a) na (b).

Mhe. Waziri ulisema kwamba vikosi hivyo vinaendeshwa na miradi mengine kama ya useremala na kilimo.

a) Jee ni viwanda vingapi vya seremala vinaendeshwa na vikosi hivyo.

b) Ni kilimo cha aina gani wanacholima cha biashara wanacholima vikosi hivyo wanavyotumia kwa ajili ya biashara ni kilimo cha aina gani Unguja na Pemba

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:**Mhe. Mwenyekiti, katika swali langu nadhani sikusema habari ya useremala kwa sababu biashara wanafanya kuwafundisha wale vijana wao hasa JKU, lakini nilisema kwamba wana Kiwanda cha Viatu na sasa hivi walikuwa na Kiwanda cha Ushoni na sasa hivi wana Kiwanda cha Viatu wanataka kutosheleza vikosi vyote viatu hapa Zanzibar.

Lakini nikasema kwamba sisi kama huwa tunashirikiana nao kwa ajili ya kuangalia sekta nyengine za kuweza wao wapate nafasi ya kuweza kutoa mafunzo kwa wale vijana wanaongia JKU lakini vile vile kuwatosheleza wao wenyewe.

Kwa upande wa kilimo Mhe. Mwenyekiti, JKU sasa hivi wana mradi wa pamoja na Serikali ya Misri, mradi huu Serikali imekubaliana kwamba upewe kipau umbele na uweze kulima vitu vya biashara wapate biashara vile vile kuweze kuuza nje, lakini zaidi wanalima kilimo cha mpunga na mahindi wanauza katika vikosi vyao na wanatumia wenyewe katika vikosi vyao.

Ahsante Mwenyekiti.

**Nam. 48**

**Kuimarisha Miundombinu ya Uwekezaji Katika Sekta ya Utalii**

**Mhe. Omar Seif Abeid** - Aliuliza**:**

Ili kuimarisha Sekta ya Utalii, kunahitajika Miundombinu mizuri pamoja na kuwawekea mazingira mazuri wawekezaji ili wavutike na uwekezaji. Na kwa sababu miundombinu ya Barabara ya kutoka Kiuyu kwa Manda hadi Makangale ni mbaya sana, kiasi kwamba hata wawekezaji na wageni wenyewe unawarudisha nyuma kutaka kuwekeza huko.

a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuimarisha barabara hiyo ili iweze kupitika kwa wakati wote kwani wakati ikinyesha mvua barabara hiyo huwa mbaya sana.

b) Je, kuna mpango gani wa kuwapa kipaumbele na kuweka vivutio maalum wenye Mahoteli ya Utalii Pemba, jambo ambalo litawavutia na kuweza kuwashawishi wawekezaji kuja kuwekeza Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo** - Aliuliza**:**

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naomba kumjibu swali lake Mhe. Omar Seif Abeid wa Jimbo la Konde Nam. 48 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo inapendelea kuwasiliana na Wizara inayohusika na miundombinu ya barabara ili kuhakikisha kuwa barabara katika maeneo ya utalii ikiwemo barabara ya Kiuyu kwa Manda zinaimarishwa ili kukidhi mahitaji ya sekta ya utalii.

b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika sekta ndogo ya hoteli katika Kisiwa cha Pemba ikiwemo kutoa vivutio kwa wawekezaji kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar ili kurahisisha uwekezaji na kuvutia wawekezaji wapya kuwekeza katika shughuli za utalii nchini mwetu hususan katika Kisiwa cha Pemba. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, na ningeomba pia Mhe. Waziri wa Fedha anisikilize vizuri pia kwenye swali langu.

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sheria za kodi kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake kwa kuwa sheria za kodi za nchi hii zote ni moja na ukiangalia katika Sekta ya Utalii masuali ya kodi ya *BOT, Hotel Levy* zote zinakwenda sambamba katika mahoteli yote. Sasa ili Pemba iendelee ni kwa nini Serikali isifikirie kuweka kodi ambazo zitakuwa zinavutia wawekezaji ili kuhakikisha kwamba Pemba nayo wawekezaji wengi ambao kutoka nchi mbali mbali waweze kujenga mahoteli kama yalivyojengwa Unguja na ya kisasa ili Serikali iweze kupata ajira pamoja na kodi.

b) Ni kweli kwamba Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar itajegwa na Wazanzibari ni utaratibu upi Mhe. Waziri anautumia kuhamasisha wakaazi kutoka Pemba ambao wengi sasa kumekuwa na desturi wanakwenda kujenga au kuwekeza maeneo tofauti kutoka kama Zanzibar Kisiwa chetu cha Unguja au hasa Tanzania Bara. Je, Mhe. Waziri haoni umuhimu na njia ambayo wataweza kuitumia nzuri ambayo itaweza kufanya hawa watu pia nao kushiriki kikamilifu katika uwekezaji wa mahoteli tofauti Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:**Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari,Utalii, Utamaduni na Michezo naomba kumjibu Mhe. Simai swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) vyote kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjiubu Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali katika kodi ambazo ziwekwa kwa uwekezaji kwa Kisiwa cha Unguja na Pemba kwani tunajua Unguja na Pemba yote tunasema ni Zanzibar na yote ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa maana hii kodi ambazo zinawekwa Zanzibar ndio hizi hizi kodi ambazo zinawekwa katika kisiwa cha Pemba. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Masoud Abrahman Masoud:**Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kwanza nimpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo kayatoa.

Mheshimiwa miundombinu ni suala pana katika kukuza utalii mbali ya ujenzi wa mahoteli, barabara na kadhalika. Je, vyombo vya habari vya SMZ kama redio zinazosikika katika *shortwave* zina nafasi gani katika vipindi mashuhuri kama vile mawiyo.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi niendelee kumpongeza Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa majibu yake, lakini pia nichukuwe fursa hii kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa ni kweli bila miundombinu mizuri hamna utalii utakao wavuti wawekezaji kuja kufanya utalii ya nchi husika, lakini kutokana na kuweka dhamira wazi ya kwamba utalii kuwa ni tegemeo la uchumi wa nchi yetu hatuna budi kuwa na suala la Mtambuka na taasisi zote ambazo zinaweza kuchangia kuendeleza vivutio vya utalii. Ni wazi kwamba Wizara kama ya Miundombinu na Ujenzi ni Wizara muhimu sana katika kuhakikisha kwamba inatengeneza miundombinu ili utalii wetu uwe na vivutio vizuri.

Kutokana na suala la vyombo vya habari Mhe. Mwenyekiti, mbali na mabarabara, ujenzi wa mahoteli na ujenzi wa vivutio vyengine vikiwemo vivutio vya michezo na vyengine, lakini vyombo vya habari navyo vina nafasi kubwa sana ya kuweza kuutangaza utalii ndani na nje.

Kwa hivyo imefika wakati kweli kwa vyombo vyetu kuweza kutangaza vipindi ambavyo vitawatanabahisha wananchi wetu na watalii walioko nje ya nchi kuona kipi kipo hapa Zanzibar katika kuutangaza utalii wetu, ni wazi kwamba redio yetu ya Zanzibar kupitia *ZBC* inasikika mbali hususan kwa matangazo ya *shortwave.* Kwa hivyo sasa imefikiwa wakati nataka nichukuwe fursa hii kuhakikisha wazi kwamba vipindi vinavyopangwa katika redio zetu vinaeleza maendeleo yanayofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa kiongozi wetu mahiri Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kufikia hayo umefika wakati sasa vipindi mashuhuri kama vile vya mawiyo vipindi vinavyosikilizwa sana na wananchi wetu viwe vinapanga mada na vipindi maalum vitakavyokuwa vinasikika huko nje ya nchi katika kueleza miundombinu yetu tuliyanayo.

Kwa hivyo ni kweli imefika wakati kuachana tu na masuala ya mawiyo kuzungumzia suala zima tu huyu kabakwa leo huyu hivi, kipindi kile ni lazima kifikie wakati sasa hivi kiwe kinatangaza mambo ya maendeleo, mambo yanayofanywa na nchi yetu na mambo yatakayo tangaza utalii, nashukuru sana.

**Nam. 112**

**Kuwekwa Maandiko Kuhusu Historia ya Zanzibar**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said -** Aliuliza**:**

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika jitihada zake ya kuiboresha sekta ya utalii ili kuongeza mapato ya Serikali lakini utalii huo umegawika katika sehemu mbili. Sehemu ya utalii wa nje na utalii wa ndani. Katika utalii wa ndani ni moja ya kuelimisha, kujua historia pamoja na elimu kwa wanafunzi na baadhi ya watu wengine ambao wanahitaji kujua historia ya Zanzibar lakini takriban historia nyingi na magofu ya Zanzibar ambayo ni kama utalii baadhi ya sehemu hazijatungiwa historia yake katika vitabu na badala yake ni mtu kujitolea kutoa maelezo anayoyajua yeye.

a) Je, ni kitu gani kilichosababisha kutofunguwa vitabu maeneo ya kihistoria hadi sasa.

b) Je, kuna mpango gani wa kuwapeleka wanafunzi kutoka katika skuli mbali mbali kutembelea na kufahamu maeneo ya historia.

c) Je, ni maeneo mangapi ya historia Unguja na Pemba yanayojulikana na ambayo hayajaandikiwa historia yake katika vitabu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo -** Alijibu**:**

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe.Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said suala lake Nam. 112 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ikishirikiana na Idara ya Mipango Sera na Utafiti katika kuanzisha kitabu ambacho kitaelezea maeneo yetu ya Kihistoria. Kitabu hicho kimo katika hatua za mwisho za kumalizika, kitapewa jina la Makumbusho na maeneo ya kihistoria Unguja na Pemba. Vitabu vya historia vipo vingi kikiwemo kitabu hicho kilichoandikwa na watendaji wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar chenye kurasa 70. Pia tunavyo vipeperushi mbali mbali vinavyotoa maelezo kuhusiana na maeneo yetu ya kihistoria.

(b) Mhe. Mwenyekiti, mpango upo skuli ambazo zinataka kupeleka wanafunzi wao huandika barua na kufuata taratibu zake ndipo huleta wanafunzi wao.

(c) Mhe. Mwenyekiti, maeneo na majengo ya kihistoria Unguja na Pemba ambayo yametangazwa katika Gazeti la Serikali ni 85 na baadhi yake bado hajaandikiwa historia yake katika vitabu kwa sababu tunafanya utafiti hatua baada ya hatua kulingana na mahitaji yanayotukabili. Mfano wa maeneo ambayo hatujayafanyia utafiti ni kama vile, Chukwani kambini Jeshini, Dunga kwa Mwinyi Mkuu, Kasri na nyumba ya Balozi wa Kingereza Chwaka, Kisiwa cha Changuu, Msikiti wa Shakani, Mahamam ya Kidichi na Kizimbani. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini katika maeneo ya skuli ambayo nimemuuliza kuhusu wanafunzi hakujibu yale ni bure au wanalipa. Lakini katika majibu yake amesema anatoa kitabu ambacho kitakuwa na kumbukumbu ya Zanzibar ambapo tayari ameseme kwamba ana maeneo mengi bado hayajafanyiwa utafiti.

Je, maeneo hayo yakishafanyiwa utafiti atayatia katika kitabu gani maana yake kama ni kitabu cha kumbukumbu alikuwa asubiri mpaka kikamilike ili akitoe kijuulikane kumbukumbu ya Zanzibar, lakini anatoa nusu nusu sijui kwa sababu gani. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Naibu Waziri ni sababu gani zinazomfanya atoe kitabu hicho kwa haraka kabla ya kufanya utafiti katika mambo yake yote.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika sehemu ambazo nimeziona ambazo hajafanyia utafiti amezionesha sehemu takriban zote asilimia mia moja ni za Unguja, Pemba sijaona hata moja ina maana Pemba hakuna au tayari zimeshaingizwa katika kitabu hicho cha kumbukumbu. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali langu mama kwamba hiki kitabu ambacho sasa hivi tumo katika matayarisho ya yale maeneo ambayo tumeyafanyia tafiti, kwa kuwa bado hakijakamilika kama nilivyosema mwanzo. Kwa maeneo ambayo hatujayafanyia utafiti tumo kuyafanyia utafiti na tutahakikisha kwamba maeneo haya yataingizwa katika kitabu hiki hiki ili kuona utafiti huu umekamilika ya maeneo yetu ya kihistoria.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwa upande wa maeneo ya skuli au kwa maeneo ya kihistoria ambayo Pemba hayaingizwa, pia kuna maeneo mbali mbali ambayo tumeyafanyia utafiti yatakuwemo katika kitabu hiki hiki yakiwemo maeneo ya Makangale yako magofu ambayo tumeyafanyia utafiti na mengineyo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Rashid Makame Shamsi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Kwanza nimpongeze sana kwa majibu fasaha ambayo ameyatoa katika swali mama.

a) Mhe. Mwenyekiti, suala la utafiti sio suala la muda mfupi ni suala la muda mrefu. Sasa suala langu utafiti huu ambao umebakia kwa maeneo ambayo ameyataja utachukua muda gani na hapo kitabu mpaka kitakuja kupatikana.

b) Mhe. Mwenyekiti, katika maeneo ambayo Mhe. Naibu Waziri ameyataja tayari watalii wa ndani na wa nje wanapita na wanapata maelezo, ina maana kwamba utafiti

ulifanyika huko nyuma. Je, maelezo haya yanayopatikana kwa watalii yatakuwa yanaaminika kiasi gani iwapo hivi sasa ndio tunaanza na utafiti. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:**Ahsante sana Mhe. wenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) yote kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nikiri kwamba suala la utafiti ni suala ambalo linakuwa la muda mrefu na lina hitaji umakini zaidi wa kufanya utafiti ule na hadi kupatikana maelezo yake sahihi.

a) Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba utafiti huu kwa vile baadhi ya maeneo ambayo yameshawekwa katika vitabu hivi na ambayo bado hatujakitoa tunaendelea na utafiti huu na ikikamilika maeneo haya atayaona katika kitabu chetu hiki.

b) Maelezo ambayo wanapewa wageni katika maeneo wanayokwenda namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba maeneo haya yamefanyiwa utafiti wa kina na yako sahihi kwa maeneo yale ya historia yetu ya Zanzibar kwa zile sehemu ambazo wageni wetu wanapita kutembelea. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 21**

**Kampeni ya Kumaliza Malaria Zanzibar**

**Mhe. Mussa Foum Mussa** - Aliuliza:

Katika malengo ya Wizara ya Afya ya kuimarisha kampeni ya kumaliza malaria Zanzibar kwa mwaka 2017/2018 ni kuongeza kasi ya kufuatilia wagonjwa wanaogundulika kuwa na maradhi hayo.

(a) Je, mpaka sasa ni wagonjwa wangapi waliofuatiliwa.

(b) Kwa kuwa kipindi kikubwa malaria yamepungua Zanzibar, kwa hivi sasa yako asilimia ngapi.

**Mhe. Waziri wa Afya** - Aliuliza:

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa na afya njema, wazima na kutimiza majukumu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam 21 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba miongoni mwa mikakati inayotumiwa na Wizara ya Afya katika kumaliza malaria Zanzibar, ama Kampeni ya Kumaliza Malaria Zanzibar ni kufanya ufuatiliaji kwa wagonjwa wanaobanika na maradhi haya katika majumbani kwao wanakoishi (*surveillance*). Ufuatiliaji wa wagonjwa

majumbani ulianza tokea mwaka 2012 na unafanyika kwa wagonjwa wanaopatikana vituo vya serikali na baadhi ya vituo vya ambavyo huripoti kesi hizi za malaria katika vituo vya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2012 hadi kufikia mwezi wa Novemba, 2017, jumla ya watu 12,899 waliogundulikana na vimelea vya malaria katika hospitali na vituo vya afya wamefuatiliwa kesi hizi za malaria majumbani mwao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafiti mbali mbali zinazofanywa juu ya kiwango cha malaria, matokea yanaonyesha kwamba kiwango cha malaria hivi sasa kiko chini ya asilimia moja. Ahsante.

**Mhe. Mussa Foum Mussa:**Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hivi sasa nchi yetu imepiga hatua ya kuondoa malaria mpaka sasa tunayo asilimia moja. Katika zile sehemu ambazo kuwa wanagundulikana wale watu wenye malaria. Je, serikali inachukua hatua gani katika vijiji vile ili kuhakikisha kwamba yanaondoka kabisa.

**Mhe. Waziri wa Afya:**Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Kwa kweli ni swali zuri sana na ni swali ambalo tunajadiliana sana baina ya Wizara yetu ya Afya Zanzibar na Wizara yetu ya Afya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kesi nyingi kila tunapofikia asilimi nusu 0.5, kesi nyingi za malaria ambazo tunafatilia hugundulikana zinatokea kwenye madago haya ya wavuvi wanaokwenda kuvua halafu wakarudi. Kwa sababu bado wenzetu Tanzania Bara malaria yao ipo kidogo juu zaidi kuliko sisi Zanzibar. Sasa katika kudhibiti hilo si rahisi kudhibiti kuwazuia watu wasiende kwenye maeneo ya malaria au watu wanaokwenda kuvua wananchi wa Zanzibar wasiende kuvua maeneo ya Bara.

Mhe. Mwenyekiti, la pili maingiliano baina ya Baraza na Zanzibar ni ya karibu sana, ni ya kihistoria, ni ya kidugu. Kwa hiyo, kuna kesi nyingi tunazofatilia ni wale wavuvi wanaokwenda kupiga dago Tanzania Bara wakakaa huko akitafunwa na mbu kwa sababu ile malaria ipo akarudi hapa, basi ile malaria huja na husambaa katika maeneo yaliyokuwa wale wavuvi wanakaa zaidi. Kwa hiyo, kuzuia moja kwa moja ni ngumu sana, tunachokifanya sasa hivi ni kufatilia *surveillance* na naamini wenzetu kule kwa kushirikiana nao kwa karibu sana Tanzania Bara, kule kidogo ni sehemu kubwa sana na malaria imetawanyika kidogo sehemu kubwa mpaka Mikoa ya ndani. Kwa kushirikiana na wenzetu naamini malaria ikidhibitiwa kufikia kule kwa asilimia iliyokuwa chini ya moja basi na huku sisi tutaweza kumaliza malaria kabisa. Kwa hiyo, ni zaidi mawasiliano baina ya Zanzibar na Bara. Ahsante.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuniona mara hii kwa sababu shingo yako ilikuwa inakuuma hukuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Zanzibar tulikuwa tunafikia karibu ya zero kuwa hatuna malaria, na kwa sababu Zanzibar ni Kisiwa watu wanaingia na kutoka mara nyingi na hatuwezi kufanya *testing* katika *Airport* wala bandarini kutokana na *nature* ya Zanzibar. Ni

utaratibu gani sasa Wizara ya Afya utauchukua ili kuweza ku-*control* malaria kwenye wasafiri ambao wanaingia na kutoka Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Afya:**Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Kama itakumbukwa zamani wakati wasafiri walikuwa wakiingia Zanzibar tulikuwa tukipewa vidonge pale *Airport* na wengine walikuwa kidogo wanafanya ukaidi wa kula vile vidonge, unapewa na *glass* ya maji na bandarini ilikuwa hivyo hivyo wakati ule wa kudhibiti malaria. Hivi sasa kwa asilimia hii tunatumia mbinu nyengine hatutumii mbinu za vidonge, tunatumia mbinu ya *surveillance* mgonjwa anapogundulikana kuwa na vimelea vya malaria tunakwenda kufatilia ile kesi na kujua mgonjwa yule alikuwepo wapi, alikuwepo sehemu gani labda nje ya Zanzibar na alikaa kwa muda gani huko mpaka kuhakikisha kwamba ile kesi ya malaria inaondoka na kudhibiti hali katika eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, kwa njia nyengine hivi sasa tumejadiliana na wenzetu pia wa Shirika la Afya Duniani, hatuwezi kurejesha ule mfumo wa zamani wa kumpa kila anayeingia Zanzibar kidonge, kwa sababu siku hizi vidonge vingi vimekuwa na *resistance,* yaani kinga ya mwili inatumika zaidi. Kwa hiyo, tunarajia hatuwezi kutoa vidonge mpaka tupime kesi ya malaria tuthibitishe kwamba mgonjwa huyu ana malaria ndipo tutoe vidonge. Kwa hiyo, yale ya zamani yote yameondoshwa kwa sababu vile vidonge vilijenga *resistance*. Kwa hiyo, njia tunayoitumia ni hiyo kwa sasa hivi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 77**

**Uhaba wa Wafanyakazi katika Vituo cha Afya**

**Mhe. Omar Seif Abeid** - Aliuliza:

Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la upungufu wa wafanyakazi kwa kada mbalimbali kwa Wizara ya Afya hasa kwa upande wa vijijini na moja kati ya tatizo hilo husababishwa na wafanyakazi hao kutokurejea kituoni kufanya kazi husingizia yupo mapumziko, lakini baadhi huwa wanafanya kazi kwa Hospitali Binafsi au "*Pharmacy*".

(a) Je, Wizara ya Afya ina mpango gani wa kuwataka wafanyakazi waliopo vyuoni wakati wa kufunga vyuo isipokuwa kama wapo "*field*" kurejea katika vituo vyao vya kazi ili kwa wakati ule wasaidiane na wenzao kufanya kazi ili kupunguza matatizo ya uhaba wa wafanyakazi.

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuwarejesha wafanyakazi waliokuwepo masomoni katika vituo vyao vya kazi badala ya kumpangia kazi sehemu nyengine na kuiacha nafasi alionayo mfanyakazi aliyemaliza masomo kuwa tupu.

**Mhe. Waziri wa Afya** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam 77 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi walioko masomoni kiutaratibu wanajulikana kwamba wako katika likizo ya masomo, hivyo kumtaka mfanyakazi huyo kurudi kazini wakati wa likizo

yake hiyo ni kuutumia muda wake ambao anatakiwa aidha kupumzika au kuutumia muda huo kwa mambo mengine ya kijamii au hata kudurusu masomo yake ili aweze kupasi mitihani yake vizuri au kutatua mambo yanayohusiana na masomo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wote wanaporudi masomoni majina yao hufikishwa katika Kamati ya Kupangia Kazi (*deployment committee)* na wafanyakazi hao hujadiliwa na ikionekana kwamba mfanyakazi husika anastahiki kurudi katika sehemu yake ya kazi ya awali basi hurejeshwa sehemu hiyo. Hata hivyo, kwa vile mfanyakazi huyo itakuwa ameongeza ujuzi basi hupangiwa kazi katika sehemu ambayo ataweza kutumia ujuzi huo. Ahsante.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Namshukuru sana Mhe. Waaziri wa Afya kwa kunipa elimu mimi na watu wengine wakafaidika, ahsante sana Mhe. Waziri. Lakini nina kijiswali kidogo cha nyongeza.

Sasa hawa wanaomaliza kusoma na wakawa hawataki kuripoti kazini kwa visingizio mbali mbali huwa mna hatua gani mnazowachukulia nyinyi ikiwa pamoja na wengine wanasema na huo muda wa kupumzika badala ya kupumzika tukawaona wanakwenda kwenye *pharmacy*. Je, kama hawa mnawachukulia hatua gani za kisheria dhidi yao. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake lake la nyongeza.

Hivi karibuni mnamo mwezi wa Januari tulifanya uhakiki kwa wafanyakazi wetu wote wa Wizara ya Afya, tuna wafanyakazi 4288 na tukagundua katika uhakiki huo tukagundua wafanyakazi 120 kwa muda wa miaka mitano walikwenda masomoni walikuwa hawakurudi kuripoti kazi. Hao wote walichukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma kuwaandikia barua, aidha kurudi kazini haraka na kurejesha pia ile mishahara ya kipindi chote ambacho walikuwa wakichukua hawakutumikia.

Aidha, tuna wafanyakazi ambao waliropiti na baada ya hapo wakaondoka bila ya kuaga kufanya kama kuendeleza ule muda wa masomo basi hatua husika wote wamechukuliwa kwa mujibu wa Sheria za Utumishi. Wafanyakazi waliogundulika kwa miaka mitano kufanya suala hilo wote jumla yao ilikuwa ni 120. Ahsante.

**Nam. 60**

**Mkataba wa Shipco na *GAPCO* Kuhusu Meli ya M.T Ukombozi**

**Mhe. Omar Seif Abeid** - Aliuliza:

Kwa kuwa Meli ya M.T. Ukombozi imekodishwa kwa Kampuni binafsi ya *GAPCO ZANZIBAR LTD* inayofanya biashara ya mafuta, kwa sababu meli hiyo hupelekwa Chelezoni Mombasa Kenya kwa ajili ya matengenezo kila mara, kutokana na kwamba Meli hio imeshakaa siku nyingi.

(a) Je, Shirika la Meli inakodisha Meli yake ya M.T. Ukombozi kwa Kampuni ya *GAPCO* bei gani kwa mwaka.

(b) Je, ni utaratibu gani unaotumika kabla ya kumpata mteja wa kukodi meli hiyo.

(c) Je, gharama za kuipeleka meli hiyo chelezoni Mombasa, huwa ni ya nani kati ya Shirika la Meli au *GAPCO* ambao huwa anakodishwa meli hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 lenye vipengele (a), (b) na **(**c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Meli liliikodisha Meli ya MT. Ukombozi kwa malipo ya Dola za Marekani 3.335.00 kwa siku. Malipo ya mwaka inategemea meli hiyo kama itafanya kazi zake kwa siku ngapi, ikizingatiwa kwamba kuna sababu nyingi za kuitoa meli hiyo katika kodi (*off hire*) na siku hizo huwa hazina malipo. Miongoni mwa sababu hizo ni;

i. Maharibiko na kushindwa kutoa huduma.
ii. Kupandishwa Chelezoni.
iii. Kuvunjika kwa mkataba kwa sababu mbali mbali.

(b) Utaratibu wa kumpata mteja wa kukodi meli hiyo ni kuchuja maombi ya kodi kutoka taasisi mbali mbali na kufungiana mkataba maalum kwa yule atakayeonekana kuwa na maslahi ya shirika

(c) Gharama za kuipeleka meli hiyo Chelezoni zinasimamiwa na kulipwa na Shirika la Meli. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Omar Seif Abeid:**Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza maswali ya nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri lakini naomba kuulize kwa kuwa gharama za matengenezo ni juu ya Shirika la Meli kama ulivyoeleza. Je, hii Kampuni ya *GAPCO* ambayo imepewa hiyo meli imekodishwa, huu mkataba wake huwa ni wa kudumu au ni wa muda gani au huwa ni wa muda tu pale anapohitaji kwenda kuchukuliwa bidhaa zake akimaliza mkataba wake ukawa umevunjika. Kama mkataba huo ni wa kudumu na unaendelea ni muda gani mkataba huu utamalizika. Je, katika kumpata huyo mteja anayekodishwa hiyo meli, huwa kuna utaratibu wa matangazo yanayotolewa ili mashirika na makampuni mengi yakapata habari kwamba kuna Meli ya MT. Ukombozi inakodishwa? Au huwa kuna utaratibu gani. Ningependa nielezwe kwa faida yangu na wazanzibari wote, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo. Mkataba wa huyo aliyeikodi Meli ya MT. Mkombozi *GAPCO* unamalizika mwaka 2018 Febuari.

Swali la pili, labda nitatoa maelezo kwa ufupi tu kwamba kabla ya hapo meli hii katika miaka ya 1990 ilikuwa iko chini ya *ECOTEC* na baadae ikaja *GAPCO* kuchukua mwaka 2000 mwanzoni. Sasa kipindi kile kilikuwa ni kampuni hizi ambazo ndio zilikuwa zinachukua mafuta. Kwa hiyo, ndio maana ukakuta *GAPCO* pekee ndiye aliyepata huu mkataba, lakini wakati wowote pale ikitokezea ushindani na sasa hivi mwaka 2018 tunamaliza mkataba basi

tutakwenda kwa mujibu wa ushindani na zabuni kwa mujibu wa ile sera yetu tuliyopitisha hivi karibuni, mwaka 2016. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 61**

**Uimarishwaji wa Miundombinu ya Barabara Kuu**

**Mhe. Omar Seif Abeid** - Aliuliza:

Kwa kuwa vipaumbele vya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ni kuzijenga barabara kuu ya Bububu /Mahonda hadi Mkokotoni na Barabara ya Wete/Chake. Kwa sababu barabara ya Msuka/Konde ni miongoni mwa barabara ambayo Mhe. Rais wa Zanzibar ameahidi kuijenga kutokana na ahadi zake za kampeni ya uchaguzi ya 2015.

(a) Je, ni lini wizara itaifikiria kuijenga barabara hiyo ambayo hivi sasa imeanza kuharibika kutokana na mvua kubwa za masika zilizopita, ukitilia maanani kwamba barabara hiyo ni ya kifusi na imeshindikana hata kuipigia mitaro ya kuihifadhi ili isimalizike kuharibika.

(b) Je, ni lini Mhe. Waziri tutakwenda kutembelea na kuona barabara hiyo jinsi ilivyoharibika na wananchi wa Msuka na Konde wanavyopata tabu na usafiri. Kwa sababu wenye magari wanashindwa kupeleka magari ya abiria kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

(c) Je, ni lini hatua za awali zitaanza kwa ajili ya matayarisho ya ujenzi wa barabara kuu za Bububu/Mahonda hadi Mkokotoni na barabara kongwe ya Wete/Chake kuanzia Mzambarautakao hadi Melitano.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Msuka/Konde ni miongoni mwa barabara zilizo chini ya usimamizi wa Wizara ya Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Hata hivyo, wizara yangu ilishirikiana na Jumuiya ya Maendeleo ya Konde kujenga daraja moja na kalvati kadhaa pamoja na kuiwekea kifusi barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 4.3, ambapo wananchi wa maeneo hayo walishiriki kikamilifu kwenye ujenzi huo na sisi tunawapongeza sana kwa kazi nzuri waliyoifanya. Gharama za mradi huo zilitotelewa na *JAICA* kwa Jumuiya ya Maendeleo ya Watu wa Konde, lakini vile vile tupo tayari kushirikiana na wizara husika pale ambapo tutahitajika kufanya hivyo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu lini nitaitembelea barabara hiyo ili kujionea hali halisi ya barabara hiyo, napenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi kwamba tayari barabara hiyo nimeshaitembelea mara mbili na ninazijua changamoto zilizokuwepo pale. Lakini hata hivyo, niko tayari kufuatana naye mara nyengine ili kwenda kujionea hali halisi.

(c) Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa barabara kuu za Bububu-Mahonda hadi Mkokotoni utaanza wakati wowote, kwani tarehe 8 Novemba, 2017 serikali ilisaini mkataba na mkandarasi aliyeshinda zabuni ya ujenzi wa barabara hiyo na nyengine tatu. Kuhusu ujenzi wa barabara kongwe ya Wete/Chake Chake kuanzia Mzambarau-takao hadi Melitano, serikali inakamilisha taratibu na wafadhili *(Saud Fund* na *BADEA)* wa mradi wa ujenzi wa barabara hiyo ya Wete-Chake Chake inayopitia Mzambara-utakao hadi Wete na pale hatua zitapokamilika basi ujenzi utaanza. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Machano Othman Said:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana lakini pia naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake. Pamoja na majibu yake mazuri nina swali moja lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Ujenzi wa barabara ya Bububu/Mkokotoni mpango wa awali ilikuwa barabara ile inaanzia Kinazini hadi Mkokotoni, lakini sasa tunasikia kwamba inaanza Kwanyanya hadi Mkokotoni. Ni sababu gani zilizosababisha mradi ule kutokuanza Kinazini na kuanza Kwanyanya na kipande hiki cha Kinazini mpaka Kwanyanya kiko hali mbaya. Itakuwaje.

(b) Pamoja na nia nzuri ya serikali na tunaipongeza sana, lakini baadhi ya wananchi wa Chuini, Mfenesini na Kama wanalalamikia malipo ya fidia kwamba hayakuwa na usawa. Waziri ana jibu gani kuhusu suala hili.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Ujenzi wa barabara ile utaanza Bububu na bado tunaendelea na mazungumzo kuhakikisha kwamba hata hapa Polisi pia kama itawezekana basi wakandarasi waendelee kuijenga kuanzia pale. Atuachie tunalifanyia kazi na nina imani kubwa sana wakandarasi wako tayari kushirikiana na sisi katika kufanikisha hili.

Kama alivyosema tulilipa fidia na hivi sasa takriban sehemu zote wameshalipa fidia na bado kuna malalamiko. Kwa hiyo, pale ambapo kuna malalamiko sisi tunawaomba wale wenye malalamiko yao watuletee ofisini na tutayafanyia kazi ili kila mmoja alipwe stahiki yake kwa mujibu wa kile kipando au nyumba yake ambayo tayari tumeibomoa au tutakichukua kipando hicho. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf:** *Bismilahi Rahmani Rahiim*. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kukujaalia kunipa swali la ziada. Nitaomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali (a), (b) na (c).

(a) Kwa kuwa barabara hiyo ya kutoka Mtoni hadi kufika jimboni kwangu Chaani na Mkokotoni itachukua takriban miaka miwili. Kwa kuwa hivi sasa jimboni kwangu wananchi hawawezi kupita mashimo mengi, njia mbovu sana na muda utakuwa mrefu mpaka kufikia njia ya Chaani. Juhudi gani atazichukua ndani ya muda huu kuhakikisha njia ile itatiwa kifusi pamoja na rojo la lami ili waweze kutumia mpaka itapofika njia ya lami kamili.

(b) Kwa kuwa kuna njia nyingi sana hapa Zanzibar zinafanya mashimo mara kwa mara na kuwa hazipitiki hasa sehemu za *airport* na mjini. Ni lini wizara yake itaanza kuweka barabara zile kwa ujenzi wa zege kama wanavyotumia nchi nyengine na kudumu kwa miaka mingi.

(c) Kwa kuwa barabara nyingi za Zanzibar mbovu hasa ukanda wa Nungwi na Kendwa na nchi hii ni ya utalii, wageni wanapotoka na safari zao wanaingia kwenye mashimo na kupata tabu gari ndogo haziingii. Ni lini wizara yake itatengeneza njia zote zinazoingia kwenye mahoteli makubwa ili utalii wetu uzidi kuimarika. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri kwa mujibu wa Kanuni jibu (a) na (b).

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mjumbe swali lenye kifungu (a), (b) na hilo jengine kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ile barabara tunajua changamoto zilizokuwepo na sisi tuliiwekea kifusi kipindi kilichopita. Lakini licha ya hivyo, bado tunaendelea na mazungumzo na mkandarasi tuangalie utaratibu gani kwamba tutaanza kwa kule au huku, lakini yote yanazungumzika. Nataka kumtoa wasi wasi tu kwamba barabara tulizokusudia kuzijenga kwa miaka miwili ni barabara zote zenye urefu wa kilomita 52, barabara kutoka Bububu/Mahonda mpaka Mkokotoni ina urefu wa kilomita 31. Kwa hiyo, nina imani kubwa sana katika kipindi cha mwaka mmoja labda na robo barabara ile itakuwa tayari imeshamalizika.

Kuhusu masuala ya mashimo kweli tunalijua hilo na kwa ufupi tu ni kwamba tayari tuna tani 50 katika tani 1,000 tulizoagiza kutoka kwa mkandarasi yule *Starpeco* na zikifika hizo tani nyengine basi tutaendelea kuziba maeneo mengine yote.

Kuhusu kujenga barabara kwa kutumia zege, hilo ni suala ambalo linazungumzika na linatakiwa kufanyiwa utafiti. Wizara yangu tunaendelea kufanya utafiti kwa sababu kumejitokeza kampuni ambazo zimeonesha nia ya kujenga kwa kutumia hiyo zege anayoisema. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umekwisha na kabla sijampisha Mwenyekiti kuendelea na shughuli nyengine naomba niwatangazie kuhusu wageni wetu wa leo, ni wageni wa Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mpendae. Wageni wenyewe ni Bwana Hassan Hamad Kasim, Bwana Amour Saleh Juma na Bwana Simai Zidi Mussa. Hawa wote ni wananchi wa Kisakasaka karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wengine wa Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Viti Maalumu Watu wenye Ulemavu. Wageni hao ni kama hawa wafuatao, hawa ni wageni wanaotoka Umoja wa Watu wenye Ulemavu ambao ni Bwana Haidar Hashim Madeweya, Bi. Mwadawa Khamis Mohamed, Bwana Haroub Said Mzee, Bwana Abdalla Abdul-Kareem Suleiman, Bi. Salma Haji Saadat, Bi Thuwaibah Shaibu Abass na Ndg. Kheir Mohamed. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mhe. Omar Seif Abeid wa Jimbo la Konde. Huyu ni Bwana Masoud Hamad Ali ni mwanafamilia anatokea Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine wa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf wa Jimbo la Chaani. Wageni hao ni Faik Fahad Idrissa na Issa Mugheir. Hawa ni wasanii wa *Cloud Bongo Movie. (Makofi)*

Wageni wengine ni wa Mhe. Shamata Shaame Khamis, huyu ni Bwana Makame Faki Ali ni Katibu Mwenezi wa Jimbo la Micheweni, pia ni Mjumbe wa Baraza Kuu la Wazazi Mkoa wa Kaskazini Pemba. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Kuna tangazo jengine la Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mhe. Mohamed Said Mohamed, ameomba kuwa wajumbe wote wa kamati hiyo wakutane saa 5 chumba namba 2. Ahsanteni sasa naomba nimkaribishe Mwenyekiti mwenza aendelee na shughuli zinazofuata.

*(Hapa Mhe. Mwenyekiti, Shehe Hamad Mattar alikalia kiti)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Katibu tunaendelea.

## TAARIFA ZA SERIKALI

### Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeanzishwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015, iliyopitishwa na Baraza lako tukufu Tarehe 30 Januari, 2015.

Sheria hiyo imetiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Tarehe 29 Mei, 2015 na kuanza kutumika rasmi Tarehe 15 Aprili, 2016, baada ya kutangazwa katika tangazo la kisheria Nam. 34 la mwaka 2016. Utekelezaji wa kazi ya tume ulianza mwisho mwa mwezi wa Aprili, 2016.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Maadili imekuwa ikitekeleza kazi zake kama ilivyoainishwa katika sheria Nam. 4 ya mwaka 2015. Ikiwemo kupokea, kusaijili na kuhakiki tamko la amali na madeni kutoka kwa viongozi wa umma. Aidha, tume inapokea malalamiko na kufanya uchunguzi kuhusu uvunjaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kutoa elimu ya umma kwa viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inahusika na masuala yote ya utawala bora katika kuimarisha juhudi za serikali za kuimarisha utawala bora. Uajibikaji na uwazi, serikali imeweka utaratibu wa kisheria kwa taasisi zinazohusika na utawala bora kuandaa na kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma inapaswa kuandaa na kuwasilisha kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha unaohusika. Kwa mnasaba huo, tume imeandaa na kuiwasilisha kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein tarehe 29 Septemba, 2017.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Dkt. Ali Mohamed Shein ameniagiza kuiwasilisha ripoti ya utekeleza wa kazi za tume kwa mwaka 2016/2017 katika Baraza lako tukufu ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako wapate fursa ya kuisoma na hatimaye kutoa maoni na ushauri wao.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii imegawika katika maeneo makuu matano, ambapo eneo la kwanza linazungumzia Utangulizi, Historia ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Dira, Dhamira, Maadili ya Msingi, Lengo Kuu, Muundo wa Tume, Majukumu ya Tume, Mamlaka na Uwezo wa Tume.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la pili linazungumzia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2016/2017, na utekelezaji halisi wa kazi za tume zilizopangwa kwa mwaka 2016/2017.

Eneo la tatu linazungumzia vikao vya tume, hali ya upatikani wa fedha, changamoto na utatuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la nne linazungumzia mikakati ya tume kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mapendekezo mbali mbali kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa kazi za tume.

Eneo la mwisho linahusu hitimisho na uwasilishaji wa ripoti.

Mhe. Mwenyekiti, matarajio yangu ni kuwa Waheshimiwa Wajumbe walipata muda wa kutosha uliowawezesha kuisoma na kuipitia ripoti hii, nina imani kubwa kuwa kwa hivi sasa wako tayari kwa ajili ya kuichangia na kutoa maoni yao ambayo yatasaidia tume katika utekelezaji wa kazi zake za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha ripoti hii kwa mujibu wa kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wako, naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

**Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum):** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, mwingi wa rehema, muumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo na kuweza kutekeleza majukumu haya muhimu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa; hali ambayo imeendelea kuipa nafasi serikali na wananchi wote kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na mafanikio. Napenda kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla tuendelee kuidumisha kikamilifu amani na utulivu huo, kwani bila ya amani hakuna maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, aidha natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kutoa maoni ya Kamati yetu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu uwasilishaji wa ripoti ya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2016/2017, kama Kanuni ya 43(1) Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2016 linavyoeleza.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua pia fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kipindi cha mwaka 2016/2017. Ripoti hii inaakisi matokeo ya kazi za msingi zilizofanywa na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma tokea kuanzishwa kwake na kuanza kufanya kazi rasmi mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje wajumbe wanaounda Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum wa Baraza la Wawakilishi. Wajumbe ni kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Machano Othman Said | - | Mwenyekiti |
| Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis | - | Makamo Mwenyekiti |
| Mhe. Wanu Hafidh Ameir | - | Mjumbe |
| Mhe. Sada Ramadhan Mwenda | - | Mjumbe |
| Mhe: Nadir Abdulatif Yussuf | - | Mjumbe |
| Mhe: Ali Khamis Bakar | - | Mjumbe |
| Ndg: Ali Alawy Ali | - | Katibu |
| Ndg: Haji Jecha Salum | - | Katibu |

Mhe. Mwenyekiti, aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa viongozi na watendaji wote wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kwa kazi zao nzuri na ngumu wanazozifanya katika kusimamia haki na uadilifu wa viongozi wa Umma Zanzibar, licha ya changamoto mbali mbali zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusiana na Ripoti hii ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar mbele ya Baraza lako tukufu kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapongeza sana juhudi za Tume ya Maadili ya Viongozi kuweza kuwasilisha ripoti yao hii kwa kipindi kifupi tu tokea kuanzishwa kwake na kuweza kuonesha mafanikio makubwa yaliyofikiwa. Mafanikio haya ni imani yangu kuwa yalipatikana kwa ujasiri na moyo wa kujitolea kutoka kwa viongozi na watendaji wote wa Tume hii.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii imeonesha kupokea na kufanya uchunguzi wa tuhuma na malalamiko ya ukiukwaji wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma, imeelezwa kuwa jumla ya tuhuma na malalamiko manne (4) kutoka kwa wananchi yamepokewa na kuweza kufanyiwa kazi. Kamati inashauri kuwa tuhuma na malalamiko ambayo hupokelewa na Tume, yaweze kufanyiwa kazi kwa wakati na haraka zaidi kwa mujibu wa muongozo wa sheria kwani kufanya hivyo kutaweza kuwasaidia viongozi wenye kwenda kinyume na sheria hii kujielewa na kujirekebisha.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia ripoti hii, Tume imeeleza mikakati mbali mbali ambayo inaitekeleza kwa lengo la kutoa elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa maadili. Kwa kutumia mikutano ya viongozi wa umma pamoja na kutumia vyombo vya habari katika kutoa elimu, Kamati inapongeza sana juhudi hizi kwa vile jamii nzima inafikiwa na kupata elimu juu ya kuwa na viongozi na watumishi wenye maadili mema jambo ambalo ndio msingi mkuu wa mafanikio katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kuwepo kwa Tovuti ya Tume ya Maadili kutazidi kuimarisha upatikanaji na utoaji wa taarifa mbali mbali ambazo zinahusiana na utekelezaji wa majukumu ya Tume. Aidha, Kamati inaridhia mpango wa Tume wa kukusudia kuingia katika mawasiliano ya mitandao ya kijamii ili kuwa karibu zaidi na jamii pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya habari nchini. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa taarifa zitakazowekwa katika mitandao hiyo ziwe katika misingi bora ya kulinda maadili ya viongozi pamoja na sifa ya viongozi husika.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, katika kukuza na kuimarisha maadili ya viongozi wa umma Zanzibar, Kamati inaipongeza Tume ya Maadili ya Viongozi kwa kuanzisha maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu. Kamati inashauri maadhimisho hayo yawe yanafanyika kila mwaka inapofika tarehe kama hii na yawe na ujumbe au kauli mbiyu ambayo itashajihisha kukua na kuimarika kwa maadili ya viongozi lakini hata watendaji na jamii kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Maadili inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zinakwaza utendaji wao. Hivyo, katika kuimarisha na kufikia malengo yaliyokusudiwa ni vyema Serikali ikaona changamoto hizi ni kizingiti kikuu na kinachopaswa kuchukuliwa hatua mapema bila kusubiriwa, hivyo, Tume yenyewe ipambane kuondosha changamoto hizi.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inatoa msisitizo kwa Tume kusimamia na kutekeleza mikakati yake ambayo imepanga kutekeleza kwa kipindi hiki cha mwaka 2017/2018, lakini mikakati hiyo itakamilika endapo changamoto walizoziainisha zitaweza kuchukuliwa hatua na kila Taasisi inayohusika kusimamia malengo ya Tume hii.

Aidha, Kamati inapendekeza kuzingatiwa umuhimu wa kuwepo kwa muundo wa Kitaasisi wa Tume ya Maadili ili kusaidia kubainisha, kuelezea na kugawa majukumu ya Tume kwa watendaji wake na kufanikisha utendaji mzuri wa kazi za Tume.

Mhe. Mwenyekiti, Pamoja na mafanikio ya Tume hiyo, Kamati inashauri kwamba ni vyema kwa Tume hiyo kuifanyia mapitio fomu ambayo inajazwa na viongozi pamoja na watendaji wa serikali kwa vile vifungu vingi  vya fomu hiyo haviendani na hali halisi ya maisha ya viongozi na watendaji hapa Zanzbar.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum inatoa pongezi zake za dhati kwa kazi nzuri za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ya kuhakikisha kwamba inasimamia maadili ya viongozi na imepata mafanikio yenye kukamilisha dira na dhamira ya Tume hii kwa muda mfupi tokea kuanzishwa kwake. Na hivyo, lengo kuu lililokusudiwa litafikiwa endapo misingi mikuu ya Maadili itazingatiwa, ambayo ni uadilifu, usiri, utaalamu, uwajibikaji na kufanya kazi kwa mashirikiano.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii, na pia nazidi kuwashukuru wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano yao makubwa waliyonipatia pamoja na kuwa na msimamo na umakini kwa wanachokisimamia.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba Kuwasilisha.(*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe ripoti imeletwa mbele yetu tunaweza kuichangia hadi sasa sijapata mtu yoyote ambaye anataka kuchangia. Mhe. Waziri hakuna hoja au.(*Makofi*)

Mhe. Waziri inaelekea hii kazi itakuwa rahisi kwako kwa hivyo karibu uendelee.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia *in sha alla* kufanya majumuisho haya haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Lakini la pili hii inadhihirisha wazi kwamba viongozi wetu Wajumbe wetu wa Baraza la Wawakilishi wameelewa vizuri ripoti yetu. (*Makofi*)

Maoni ya Mwenyekiti, tumeyasikia, ushauri wake tumeusikia *na in sha alla* tukijaaliwa tutayafanyia kazi. Ashante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Wajumbe, sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na ripoti ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**HOJA ZA WAJUMBE**

**Kuweka Miundombinu Bora kwa Watu wenye Ulemavu katika Majengo Barabara Makaazi, Maeneo ya Kupumzikia na maeneo mengine.**

**Mhe. Mohamed Said Mohamed:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kusimama kwenye Baraza lako tukufu. Lakini nimuombe Mwenyezi Mungu sana anipe hatua njema nikisima kwenye Baraza lako tukufu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya msingi kikatiba. Lakini vile vile niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpendae kwa kuendelea kuniunga mkono na mimi niwaambie tu kwa lugha nyepesi sana sitawaangusha.

Vile vile nitoe pole kwa wanajeshi wetu wote pamoja na wa jimbo langu waliofariki kule DRC Congo. Msiba huu ndio msiba wetu wa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, baada hayo machache sasa naomba nitoe maazimio kuhusu kuweka kanuni na viwango vya miundombinu ya lazima inayohusu miundombinu ya majengo barabara makaazi, maeneo ya kupumzika na maeneo mengine mbali mbali ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kuweza kuyafikia kwa urahisi na kupata huduma na fursa hii haki na usawa katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja hii chini ya kanuni ya 27 fasiri ya 1(n) na kanuni ya 27 fasiri wa 3, kanuni ya 49 fasiri wa kwanza na kanuni ya 50 ya kanuni ya Baraza la Wawakilishi toleo ya 2016.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya hoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa juhudi kubwa za kilimwengu katika kushughulikia maswala mbali mbali mtambuka hususan kuhusu haki, fursa  na usawa katika kuwapa wenzetu wenye ulemavu ambao ni muhimu katika kujumuisha michango wao wa ujenzi wa taifa letu kwa dhana kubwa ya walezi si kutoweza bali ni kuweza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na mikataba mbali mbali ya kimataifa inayolinda haki za wenzetu wenye ulemavu ambayo imetowa haki, fursa, usawa ikiwemo haki ya kuweza kufikia huduma za kijamii kwa kuweko miundombinu rafiki ya majengo maeneo ya sehemu zenye maeneo na huduma hizo. Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imerihidia mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu *UN Convention on Right of Person with Disability* ambao umetowa haki hizo mbali mbali ikiwemo haki ya watu wenye ulemavu kupata fursa na kupata huduma za kijamii kwa kuweko miundombinu rafiki majengo yanayowezesha kufikia huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa mkataba huo wa Umoja wa Mataifa wa haki za watu wenye ulemavu umefafanua kuwa nchi washiriki katika kusaini mkataba huu zinahakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanaishi kwa kujitegemea na kushirikishwa kikamilifu katika nyanja zote za maisha. Aidha nchi hiyo hizo zitakazosaini mkataba huu zitalazimika kuchukuwa juhudi za lazima kuwawezesha watu wenye ulemavu kuzifikia kwa usawa huduma za kijamii katika maeneo yote. Huduma ya usafiri, mawasiliano, teknolojia pamoja na huduma nyengine za kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hatua hizo  zinazotakiwa kuchukuliwa zinataka kuondolewa kwa vikwazo vya vizuizi vyote vinavyofanywa na watu wenye ulemavu kushindwa kufikia huduma hizo. Nchi zilizosaini mkataba huo zimelazimika kuhakikisha kuwa miundombinu ya majengo, barabara, usafiri, huduma za kijamii ndani na nje kama vile elimu, afya maeneo ya kazi mawasiliano huduma za kielektroniki  na hali ya dharura ziwe zinaweza kufikiwa na watu wenye ulemavu bila ya kuwepo na vizuizi vyovyote.

Na kwa kuwa miongoni mingine mbali mbali ya kitaifa imeweka mkazi kwa nchi wanachama Umoja wa Mataifa kuteleza kwa vitendo maazimio hayo ya kuweka viwango maalum vya usawa, upatikanaji wa huduma hizo za watu wenye ulemavu kwa kuondolea vizuizi na vikwazo vya kufikia huduma za kijamii kama ilivyoelezwa katika kipengele cha 5 cha Muungozo wa Umoja na Mataifa ulioweka viwango vya usawa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa misingi hiyo ya usawa wa tu wenye ulemavu inakwenda sambamba na Azimio la kilimwengu la haki za binadamu ambalo katika kifungu cha kwanza kimeeleza kuwa binaadamu wote huzaliwa huru na haki ya kupata heshima ya binaadamu na haki sawa katika kuishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu ya Zanzibar kama sehemu ya kilimwengu imekuwa ikungana na juhudi hizo za kuhakikisha wenzetu watu wenye ulemavu wanapata fursa, haki na usawa katika nyanja mbali mbali za kimaisha kama vile afya bora, elimu, ajira, michezo na kushiriki katika ngazi mbali mbali za uongozi na kufanya maamuzi yanayoamua mustakabali wao na taifa kwa jumla. Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara imeweka misingi ya haki usawa kwa watu wote bilaya ubaguzi na kutoa fursa sawa kwa wananchi wote kuweza kupata na kufikia haki na fursa mbali mbali za kijamii bila ya kubaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ya Zanzibar imekuwa na sera na kutunga sheria ya watu wenye ulemavu haki na fursa. Sheria namba 9 ya mwaka 2006 ambayo imeweka masharti ya haki na fursa za watu wenye ulemavu katika vifungu vya 12 na 13 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 kinaeleza na naomba ninukuu kwa ruhusa yako.

> "Watu wenye ulemavu watakuwa na haki ya kutopata kizuizi, kuwa na mazingira rafiki yatakayowezesha kuwa na fursa rafiki katika nyumba za umma na vifaa kwa ajili ya matumizi ya umma, barabara mambo mengine ya burdani na vifaa visaidizi na na vyombo vyengine vya kuwezesha kutembea".

Masharti ya kifungu cha kwanza cha kifungu hichi yanatumika na kuwabana wamiliki wa majengo ya umma yaliko na huduma kwa matumizi ya umma, barabara na mambo mengine ya burdani miezi 12 baada ya sheria hii kuanza kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, wasanifu wa majengo, wahandisi wa ujenzi na watu wengine wanaohusika na usanifu wa ujenzi wa majengo wanalazimika kuzingatia upatikanaji wa vifaa wakati unaanza utaratibu wa kuandaa michoro hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhakikisha kwamba majengo yote yanaenda sambamba na michoro yenye lengo la kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 13 kinaeleza kama ifuatavyo na naomba nikinukuu kwa ruhusa yako.

> "Waziri anaweza baada ya kushauriana na mawaziri wanaohusika na usafiri, mawasiliano, nyumba na michezo kwa kutunga kanuni kuweka viwango na miungozo kwa watu wenye ulemavu kuwawezesha kufikia vyombo vya usafiri wa umma vituo vya vyombo sehemu za kusimama huduma za majengo ya umma vituo vya michezo na sehemu nyengine za burdani.
>
> Sharti la upatikanaji wa viwango hivyo itajumuishwa pia katika michoro na ujenzi wa mazingira yenyewe. Waziri kwa kushauriana na Baraza kwa kuweka utaratibu wa kukagua na kufuatilia na kuhakikisha utekezaji wa viwango na miongozo iliyowekwa chini ya kifungu cha 13"

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tokeo kutungwa katika sheria hii mwaka 2016 utekelezaji wa masharti hayo umekuwa ya kiwango cha chini kwa vile bado wenzetu wenye ulemavu mbali mbali haswa ulemavu wa viungo na uoni ambao wamekuwa wakisumbuliwa katika kufikia majengo ya umma na binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa bado yapo majengo mbali mbali yamejengwa baada ya kutungwa sheria hii mwaka 2006 yalitakiwa kujengwa kinyume na masharti ya sheria hii na kusababisha changamoto kwa wenzetu wenye ulemavu.

Aidha masharti ya kifungu cha 12 na 13 cha sheria hii ni wajibu wa serikali kuhakikisha yanatekelezwa kwa kuwa mamlaka ya utekelezaji hayo yamewekwa mikononi mwa mawaziri waliotajwa katika vifungu hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa kumekuwepo kwa miongozo na viwango vya kuhakikisha huduma hiyo inapatikana katika miundombinu ya majengo husababisha usumbufu mkubwa kwa wenzetu wenye ulemavu kwenda kinyumke na mikataba ya kimataifa na miongozo iliyotajwa hapo mwanzo. Kwenda kinyume kwa Katiba, Sheria yenyewe iliyotungwa na Baraza hili tukufu mwaka 2016 kuendelea kuwanyima fursa na haki wenzetu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia tu katika jengo letu la Baraza la Wawakilishi sasa hivi ndugu zangu wenye ulemavu walikuwa wakipata tabu sana kuweza kupanda hata angalau juu kuweza kutusikiliza.

Lakini jambo jengine uliona jinsi gani watu hawa waliokuwa wakipata tabu ulipokuwa ukiwaita pale kuwatambulisha walishindwa hata kunyayuka kwa haraka. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo basi mimi Mohamed Said Mohamed  Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia Jimbo la Mpendae chini ya kanuni ya 27 fasili ya kwanza (n) na fasili ya 27 na kanuni ya 49 na ya 50.

Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2016 naliomba Baraza lako tukufu lipitishe maazimio haya kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa hapa nataka tusikilizame kwa pamoja na tuone maazimio haya kwa wenzetu wenye ulemavu na ikisha tuweze kuyachangia vizuri sana.

**Azimio ya kwanza**,
Serikali kutekeleza kikamilifu na kwa vitendo masharti ya kifungu cha 12 na cha 13 cha sheria ya watu wenye ulemavu haki na fursa na  sheria namba 9 ya mwaka 2009 ambayo imetungwa na Baraza la Wawakilishi pamoja na masharti mengine sambamba na vifungu hivyo.

**Azimio la Pili,**
Kutungwa kwa kanuni na kuweka viwango na miongozo kwa watu wenye ulemavu kuwawezesha kufikia vyombo vya usafiri wa umma, vituo vya vyombo hivyo, sehemu za kusimama, huduma za majengo ya umma, vituo vya michezo na sehemu za burudani.

**Azimio la Tatu:**
Kwamba wamiliki wote wa majengo yote yaliyopo ambayo hayana miundombinu rafiki ya kuwawezesha walemavu kuyafikia, wabanwe na serikali kama sheria hii inavyoagiza. Wafanye marekebisho ya miundombinu hiyo ili watu wenye ulemavu waweze kuyafikia.

**Azimio la Nne:**
Serikali iwatake wasanifu wa majengo, wahandisi wa ujenzi na watu wengine wanaohusika na usanifu na ujenzi wa majengo kuzingatia sharti ya Sheria ya Watu wenye ulemavu wanapoona na kuandaa michoro na kuhakikisha majengo mapya yanakuwa na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Aidha serikali isitoe kibali cha ujenzi wowote mpya usiozingatia masharti ya sheria ya kuwa na miundombinu rafiki kwa walemavu.

**Azimio la Tano:**
Ukaguzi maalum ufanywe na serikali katika kuhakikisha kuwa majengo ya ujenzi wowote unafanyika kwa kuzingatia masharti ya sheria ya watu wenye ulemavu yanatakiwa kuwepo miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sasa naomba niseme tu Waheshimiwa Wajumbe waweze kuijadili hoja hii na baadaye tuweze kupitisha maazimio haya yote matano niliyoyataja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana sasa naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa Wajumbe tuko tayari kuijadili. Hapa ninae Mhe. Mwantatu Mbaraka wa Viti maalum kuweza kutoa mchango wake.

**Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kuwa mtu wa kwanza kuchangia hoja hii ambayo imewasilishwa mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Mohammed Said (Dimwa) kwa kuona shida na dhiki zinazowapata watu wenye ulemavu kutokana na miundombinu isiyorafiki na akaweza kuleta hoja hii mbele ya Baraza hili Tukufu ili tuweze kuichangia.

Mhe. Mwenyekiti, kitendo hichi alichokifanya Mhe. Dimwa kinafaa kuigwa na Wajumbe wengine na kwa vile tunaelekea katika jamii jumuishi. Suala la watu wenye ulemavu katika Baraza sio lazima lizungumzwe na Mwakilishi wa watu wenye ulemavu. Kitendo alichokifanya Mhe. Dimwa ni cha kupongezwa, kwa sababu yeye hawakilishi watu wenye ulemavu lakini ameona kwamba yumo katika sehemu ya jamii na akaona hili suala linagusa jamii moja kwa moja na aweze kuliwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti, katika malengo 17 ya Dunia *(Sustainable Development Goals)* lengo la 16 limezungumzia *inclusive society*. Pamoja na mambo mengine pia yamezungumzia *inclusive society.* Hatuwezi kuwa na jamii jumuishi bila ya kuondoa vikwazo vilivyopo ambavyo vinamfanya mtu mwenye ulemavu kushindwa kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja na kuwepo Sheria Nam. 9 ya mwaka 2006 na vile vile Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu, lakini bado kuna changamoto kubwa inayowapata watu wenye ulemavu katika kufikia majengo mbali mbali ambayo yanatoa huduma za kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, watu wenye ulemavu wanahitaji kujumuika na wengine wasio na ulemavu kwani ni haki yao ya msingi kushiriki katika shughuli mbali mbali za kijamii. Kutokana na mazingira yaliyopo hivi sasa, haki hii inakosekana kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, tuchukue mfano wa jengo letu hili pamoja na kuwa malengo yale 17, lile lengo la 16 limezungumzia *inclusive institution*. Tukiangalia hii *institution* ambayo jamii yote inatakiwa kuja hapa. Jengo hili limejengwa baada ya kupitishwa sheria hii mwaka 2006. Lakini tukiangalia mazingira yake sio rafiki kwa watu wenye ulemavu. Hii leo kuna wengine wameshindwa kufika hapa kutokana na mazingira yalivyo na kwa wale waliofika hapa ilibidi wabebwe ili waweze kufika kule, kitendo ambacho kinamnyima haki ya uhuru wa mtu, haiwezekani mtu mzima kubebwa mbele za watu lakini hii inatokana na miundombinu ambayo haiko sawa mpaka sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, si hilo tu kuna jengo la *ZSSF* limejengwa baada ya kupitishwa sheria hii, jengo lile tuna hamu watu wenye ulemavu tuweze kutumia jengo lile lakini kutokana na mazingira yaliyopo jengo lile watu wenye ulemavu wanashindwa kulitumia. Huo ni mfano

kwa taasisi hizo tu ambazo nimezitoa. Lakini pia kuna taasisi nyengine ambazo za umma na zisizokuwa za umma, pia zinakuwa na mifano kama hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo suala la miundombinu ya majengo bado ni changamoto kubwa na niseme kwa kweli kwa watu wenye ulemavu linatupa shida sana na nathubutu kusema nataka jamii ielewe kwamba jamani anayevaa kiatu ndiye anayejua kwa namna gani kinambana. Kwa hivyo tunapopiga kelele tunakasema jamani miundombinu haiko rafiki lazima tueleweke kwamba kweli tunakuwa tunakwazwa na hiyo miundombinu ambayo iliyopo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona jitihada za Serikali hasa Wizara ya Elimu kufanya marekebisho ya majengo kwa kuweka *ramps* lakini tatizo lililokuwepo *ramps* zile zimewekwa tuu mtu kaweka, bada la ya kuondoa tatizo zinaongoeza tatizo kwa sababu *ramps* zile zinajengwza hazina viwango maalumu. Kwa hiyo ushauri wangu kwa wale ambao wanajenga zile *ramp* kwa ajili ya marekebebisho ili watu wenye ulemavu waweze kutumia majengo yale, basi waweze kufuata vipimo vya kitaalamu ambavyo vimewekwa ili waweze kufanikisha lile ambalo wamekusudia kwa nia njema kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, katika malengo hayo hayo 17 ya maendeleo endelevu kumeelezwa ujumuisho wa masuala mbali mbali ya watu wenye ulemavu katika mazingira haya ujumuhishi haupatikana na wala hautopatikana. Hivyo basi Serikali kwa sasa itunge Kanuni zitakazowezesha Sheria yetu namba 9 ya mwaka 2006 iweze kutekelezeka na kila taasisi iweze kutekeleza majukumu yake vyema, lakini pia kutokana na kuwa mara nyingi kanuni huwa zinachelewa basi ni vyema Serikali ikachukua hatua kwa wale ambao wanaikiuka hii sheria na kujenga majengo ambayo yana vikwanzo kwa kutumia watu wenye ulemavu, niombe Serikali ichukuwe hatua ya kuyavunja majengo hayo ili kutoa fundisho kwa wengine waweze kuzifuata sheria ambazo zimetungwa.

Mhe. Mwenyekiti, miundombinu ya barabara pia ni tatizo kwetu sote ni mashahidi kwa wale wasio na ulemavu wanakuwa wanapata tabu sana kutumia barabara zetu, kwa sababu barabara hiyo wanapita wanaoendao kwa miguu wanaopita wanaoenda na baiskeli, wanaoenda na pikipiki lakini na magari na fujo sote tunazijua za barabarani. Mara nyingi zinatokea ajali kwa watu wenye ulemavu kugongwa na wengine kupoteza maisha kutokana na hali zao. Hivyo, ningeiomba Serikali wanapotengeza barabara au kufanya matengenezo ili wakaweka sehemu ambazo watu wenye ulemavu wataweza kupita bila ya matatizo, naamini tukikubali kwa pamoja na tukizingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu naamini kwa serikali yetu sikivu hili litawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mchango huo naunga mkono maazimio yote yaliotolewa na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) katika hoja yake.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe. Mhe. Waziri kwa niaba ya Waziri husika endelea kutoa maoni yako.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko (Kny: Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Mwenyekiti, nilijaribu kusimama kwa sababu kwa taratibu za sheria, hoja yoyote inapotokea lazima Serikali au Waziri anayehusika atoe maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Kaimu Waziri wa Ujenzi na Naibu wangu yupo pale naomba nitoe maneno kidogo kuunga mkono au kutoa maelezo ya ziada kuhusu hoja hii. Serikali haina tatizo na hoja hii ni hoja ya msingi na ni hoja muhimu kwa sababu Serikali yetu ipo katika mstari wa mbele kutekeleza na kutoa fursa na kuhakikisha kwamba haki za watu wenye ulemavu wanapata bila usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwakumbushe tu Waheshimiwa Wajumbe kama mwaka 2006 kama ilivyosomwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) Serikali yetu ilipeleka sheria hii na ikaunda Idara Maalum ya Walemavu, wakati huo mimi binafsi ndiyo niliyopitisha sheria hii na nilikuwa Afisi ya Waziri Kiongozi. Kwa hiyo ni ishara tosha ya kuhakikishia ndugu zangu watu wenye ulemavu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawajali na iliowapeleka mara ya kwanza kwenye mikutano ya Umoja wa Mataifa rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekubali na imeridhia maazimio yote, makubaliano yote yanahusu watu wenye ulemavu. Lakini pia ndani ya Katiba yetu pia imeweka haki za msingi zao wananchi wote wakiwemo watu wenye ulemavu, vile vile kama nilivyosema kwa mujibu wa Sheria ya 2006 Namba 9 tulishatoa muuongozo kama serikali rasmi kwamba watu wenye ulemavu waweze kupata *access* ya majengo, usafiri na maeneo mengine yote, huo muongozo umetolewa na unafanyiwa kazi.

Sasa haki ya kuwa na fursa zote kama nilivyosema pale mwanzo kuwa na mazingira rafiki walemavu wapate vifaa, tutaendelea kusimamia kama Serikali na vile vile kama Wizara inayohusika kwa sababu Serikali inawajali watu wenye ulemavu lakini pia Serikali inataka kutekeleza makubaliano na maazimio sio tu ya kitaifa, lakini kubwa ambalo tulilifanya kwamba kuchukua yale maazimio na makubaliano ya kimataifa kuyafanya kuwa sheria na ndio maana hii Sheria ya 2006 ikaweka mambo yote ambayo Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) ameyaeleza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie kwa upande wa serikali kwamba tutachukua hatua kama hivi hoja ilivyokuwa imeelezwa. Kwa sababu hoja hii ilichofanya ni kutukumbusha na kutilia mkazo, kwa sababu inaweza kuwa kuna baadhi ya maeneo bado utekelezaji wake haujaweza kuwa kikamilifu. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie mtoa hoja na Waheshimiwa wote Wajumbe wa Baraza hili na wananchi, Watu Wenye Ulemavu ambao wanatusikiliza kwamba tunakubaliana na hizi hoja.

Hoja ya kwanza kwamba twende kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 2006, lakini hoja ya pili, ya tatu, ya nne na ya tano inatukumbusha kwamba tuweke viwango, tuweke kanuni, tufuate viwango, tufuatilie hata kwenye daladala kuona kwamba watu wenye ulemavu wanapata kupanda gari bila ya usumbufu na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niseme tu kwa niaba ya Waziri anayesimamia Wizara hii na kwa niaba ya serikali kwamba hoja hii imekuja kwa wakati wake, serikali hatuna mgogoro na hoja hii. Kwa sababu watu wenye ulemavu ni wananchi wetu na tunawapenda na tunawataka na wao wajihisi kama ni watu kama walivyo watu wengine.

Natoa mfano, kuna sheria sasa hivi ambayo wenzangu wenye ulemavu hawajui inaitwa *Marrakesh Protocol* ambayo inataka watu wenye ulemavu sio tu kwa upande huu, lakini hata vitabu wanavyosoma, hata maandishi ya biashara na kadhalika wapewe kwa utaratibu wa maandiko ambayo watu wenye ulemavu wanaweza kuyafuata.

Kwa hiyo, naomba nimalizie kwa kusema kwamba hoja hii imekuja kwa wakati wake mzuri na serikali itaifanyia kazi. Tunataka watu wenye ulemavu na wao wajihisi kwamba ni watu ambao wanathaminiwa na serikali, inawapa haki zao kama ambavyo tumekubaliana kwenye Katiba na kwenye maazimio yote ya kitaifa na kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyeikiti:** Waheshimiwa Wajumbe maoni ya serikali tumeyasikia tunaendelea na mjadala wetu. Mhe. Panya Ali Abdalla wa Viti Maalum aendelee kwa kutoa maoni yake.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote na mimi sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana katika Baraza lako hili tukufu.

Pia nichukue fursa hii kukushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza na mimi kunipa nafasi...

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe kama tunavyojua ukumbi wetu una *echo*, kwa hivyo lengo la kusimama mjumbe kutoa hoja zake na maoni yake ni kwamba yasikilikane. Kwa hivyo, tupunguze sauti za minong'ono ili mjumbe asikilikane nini anachokichangia. Ahsante.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa hii nizungumze machache kuhusu hoja hii ambayo ametuletea kaka yetu Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mheshimiwa na mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa kuona na kwa umahiri alionao kuweza kuileta hoja hii mbele yetu. Hii hoja ni yetu sote, inatugusa sote kwa sababu mtu yeyote anaweza akawa mlemavu wakati wowote sio lazima mlemavu aliyezaliwa tu, kuna ulemavu wa ugonjwa mtu anaweza kupata maradhi na akapata kuwa mlemavu na anaweza kupata ajali wakati alikuwa mzima na akawa mlemavu. Kwa hivyo, hii hoja ni yetu sote na nampongeza sana Mhe. Mohamed Said kwa kuliona hili, kwa sababu usitengeze jambo labda kwa fulani, lakini hili linatugusa sote kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuipongeza sana serikali kwa juhudi kubwa wanayoichukua ya kuhamasisha na kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuwafichua watoto wenye ulemavu ambao wana haki na fursa sawa na mtu mwengine yeyote ili watu hawa waje kupata elimu na mahitaji mengine yote yanayowahusu kama binadamu wengine wanavyopatiwa mahitaji. Mheshimiwa serikali naipongeza sana kwa sababu inachukua juhudi kubwa ya kuwatafuta na wakisikia habari kuna mtu ameficha mtoto mwenye ulemavu, basi wanachukua juhudi ya kwenda na kufuatilia ili waone mtoto huyo au mtu huyo anapata haki yake ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niseme na naungana na Mhe. Mohamed Said Mohamed kwanza katika yale maazimio yote ambayo ameyatoa ni kweli, ni sahihi. Lazima sasa serikali ijipange kuhusu kuona inatengeneza miundombinu rafiki ambayo itawawezesha wenye ulemavu mahala popote kuweza kuingia na kupata mahitaji yao.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyotangulia kuchangia mjumbe wa mwanzo kabisa Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis alisema, hili jengo letu la Baraza la Wawakilishi ambalo hapa ni

pahala kwanza wanapoingia wageni wengi, lakini hapa ndipo zinapopita bajeti zote za serikali. Sasa jengo hili lilitakiwa liwe ni mfano, ni kioo cha mwanzo kuona tumetengeneza miundombinu ambayo itamuwezesha mtu yeyote.

Mheshimiwa tumekuwa tukishuhudia Mkurugenzi wetu wa Watu Wenye Ulemavu hapa anayekuja anapata shida sana kupanda wakati wa bajeti anapohudhuria katika Baraza hili. Lakini tuone kwamba hiki chombo wageni wengine wowote wanaweza kutokea na wakahisi bado pamoja na sheria tuliyoiweka, pamoja na sera ambayo tunayo kuhusu watu wenye ulemavu basi bado hatujaweza kukidhi yale mahitaji yao kama yanavyotarajiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niseme au niiombe sana serikali kuweza kujitahidi kuweka miundombinu ambayo iko rafiki kabisa na watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo nayo yeye ni mlezi wetu, yeye ndiye msimamizi wetu katika shughuli zote za serikali. Kwa hivyo, ofisi hiyo nayo na watu wenye ulemavu ni taasisi ambayo imo katika ofisi yake. Kwa hivyo, mimi naomba sana serikali ingeliona jambo hili kuliangalia kwa mtazamo uliokuwa mkubwa na mzuri wakaweza kuiweka miundombinu iliyokuwa rafiki ambayo itaweza kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaye mkurugenzi wetu pale utamuona anavyopata shida. Kwa kuwa serikali inawajali na inawahamasisha watu watoke, basi naomba sana lazima miundombinu iwe rafiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba watu wenye ulemavu pamoja na kuwatengenezea miundombinu ya majengo, barabara na kila kitu. Lakini watu wenye ulemavu wameonesha juhudi kubwa ya kujiendeleza katika elimu. Kwa hivyo, naomba wale ambao wameweza kusoma na kupata vyeti kama walivyo wenzao wengine, basi mahitaji ya kazi yanapojitokeza na wao waweze kufikiriwa na kupatiwa kama watu wengine wanavyopatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tumeshuhudia hata hivi juzi tu tumewaona watu wenye ulemavu wanashiriki katika michezo tofauti. Kwa hivyo, ni lazima sasa tukubaliane ili tuweze kwenda nao sambamba. Tena niseme watu wenye ulemavu wanatupita saa nyengine hata sisi wenye viungo vyetu kamili. Ni wabunifu na ni watengenezaji wa vitu vizuri. Kwa hivyo ni lazima sasa tujielekeze ili kuona na wao tunawapatia mahitaji na tunakwenda nao sambamba, tukizingatia kwamba ulemavu anaweza kupata mtu mwengine yeyote na akaweza na yeye kuingia katika kundi lile na akaweza na yeye kupata huduma. Mhe. Mwenyekiti, kwani unapolitengeneza jambo sasa hivi basi baadae linakuja kuwa msaada kwako. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba sana na naunga mkono kwa asilimia mia moja hoja hii ya Mhe, Mohammed Said Dimwa, na wajumbe tuichangieni hii ni hoja muhimu sana na tunaiomba serikali iweze kuzingatia na iweze kutekeleza kwa vitendo kabisa yale maazimio ambayo Mhe. Mohammed Dimwa ameyaweka ambayo yatakuwa ni rafiki kabisa kwa watu wenye ulemavu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Rashid Makame Shamsi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuweza kuichangia hoja hii ya mjumbe wetu Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa inayohusiana na fursa ambazo ingebidi kutolewa juu ya wenzetu watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kwanza kama walivyotangulia kusema wenzangu kuweza kumpongeza sana Mhe. Mohammed Said Dimwa, kwa kufikiria kuweza kuleta hoja hii Barazani. Imani yangu ni kwamba hakupata shinikizo lakini yumkini na yeye amejiona kwamba ni mlemavu mtarajiwa wakati wowote. *(Makofi)*

> Mhe. Mwenyekiti, lakini tukubali kwamba kama alivyotangulia kusema Mjumbe aliyepita dada yangu Mhe. Panya kwamba mwanadamu yeyote hata aliyekamilika ni mlemavu mtarajiwa. Kwa hivyo, ni vyema lazima tuwe na hisia juu ya suala zima la ulemavu, kwa sababu sote tupo katika kapu moja sasa hivi au halafu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la wenzetu watu wenye ulemavu juu ya kuwepo kwa miundombinu rafiki kuhusiana na majengo, barabara na nyanja nyengine zote ikiwemo viwanja vya michezo ni suala ambalo lina historia ndefu. Hivi sasa tutakapokuwa tunazungumza suala la kufikiria miundombinu rafiki kwa wenzetu wenye ulemavu, basi lazima tujiulize tunatoka wapi. Tatizo kubwa sana ambalo limechangia mpaka hii leo Mhe. Mwenyekiti, ni mitizamo yetu sisi wanadamu. Katika majengo mengi na miundombinu mingi ambayo tumerithi kutoka hata ukoloni, basi mingi yao haikuweza kuzingatia wenzetu wenye ulemavu. Kwa hivyo, kuna baadhi ya majengo ambayo hivi sasa ni ofisi za serikali lakini yamerithiwa na miundombinu mengine ambayo haikuzingatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo ni wakati ambao umefika sasa hata kwa yale majengo ambayo tumerithi, kwa kuyatumia wakandarasi wetu kama inawezekana basi tufanye *modification* ili yaweze kuwasaidia wenzetu wenye ulemavu. Kwa kweli hali ya miundombinu kwa asilimia kubwa haizingatii wenzetu, pamoja na kufuata matoleo mengi, maazimio mengi ya kimataifa, lakini bado tukitizama kiasilimia basi hatujafika hata asilimia 40 juu ya kuzingatia suala la miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu, kwa hivyo wakati umefika.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili sio la serikali peke yake. Mhe. Mohammed Said Dimwa ameelekea zaidi katika serikali, serikali ni watu na watu ndio sisi. Mhe. Mwenyekiti, sisi wanadamu ni wadhaifu sana, sisi tunasahau hata siku ya kufa. Kuna baadhi ya nyumba, wewe uliyeijenga nyumba siku ile ambayo umekufa basi uvunjwe mlango ndio tusi lipitishwe. Huo ni ushahidi ambao unatokea katika majumba mengi, sasa seuze watu kama wanakumbuka ulemavu, ile kufa yake anasahau, nyumba inajengwa mpaka tusi yake basi inashindikana kupitishwa. Sasa suala hili sio suala la serikali peke yake ni suala la kutazama sekta binafsi yenyewe, majengo mengi ya biashara yanayojengwa na sekta binafsi basi hayazingatii watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, ukitazama magari ya daladala, basi daladala nyingi ambazo zinakuja hapa kama *second hand*, tokea kwao ziliangalia watu wenye ulemavu lakini tukija hapa tunazifanyia *modification* zinawasaidia zaidi wale ambao wana miili yao kamili. Sasa hapa tunakwenda wapi, umeinunua gari kule miundombinu yake ilikuwa inaruhusu mlemavu aweza kupanda, lakini inapofika hapa unaibadilisha mlemavu hawezi kupanda. Sasa ni suala sio la serikali tu, lakini na kutazama hata na sisi wenyewe wanadamu, sisi wenyewe wananchi wa kawaida kuweza kutazama haya masuala. Kuna masuala yamo ndani ya uwezo wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na upungufu wa alama za barabarani zinazowarahisishia watu wa kawaida na watu wenye ulemavu kuweza kukata. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tujiulize mtu yuko katika *zebra cross* dereva anakuja wangu wangu seuze mlemavu ni suala letu wenyewe, yaani hata sisi wenyewe hatujali. Sasa hata ungeweka *zebra cross* ngapi, kama sisi wenyewe

hatujabadilika kimtazamo kwamba ni walemavu watarajiwa, basi tusitarajie serikali itafanya kila kitu. Kwa kweli tunalazimika sisi wenyewe wananchi kwa sehemu kubwa tuweze kubadilika kimtazamo juu ya suala la wenzetu wenye ulemavu, vyenginevyo tutakuwa tunailaumu serikali kila mara juu ya hili. Serikali iwe na upande wake juu ya sera na majengo ya ofisi zake, lakini kwa upande wa sekta binafsi nayo lazima iweze kutazama miundombinu ile ambayo wanatolea huduma. Iwe ni *dispensary*, iwe ni hospitali binafsi, iwe ni majengo ya biashara na kadhalika. Lakini hata magari yetu ambayo tunawapa madereva wetu kuweza kuwachukua wanachi, basi hili vile vile tuweze kulitizama.

Mhe. Mwenyekiti, lakini na majumba yetu sasa, nilitoa mfano ule wa kusahau kufa kwako, lakini unasahau kwamba iko siku unaweza ukawa mlemavu. Hiyo nyumba uliyoijenga inaweza kukuwezesha, basi kama tutaangalia majumba yetu mengi basi sisi wenyewe hayawasaidii watoto wetu ambao wana ulemavu. Kwa hivyo, ni suala la taifa na ni suala la kila mwananchi kuweza kubadilika juu ya hili.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika miundombinu ya vyoo. Pamoja na majengo tuliyoyarithi basi hata zile sehemu za chini ambazo zinafikika basi tuone kwamba kuna vyoo ambavyo wenzetu walemavu wakifika pale vinaweza kuwasaidia. Lakini hata hili katika yale majengo ambayo pengine juu hawezi kupanda, basi hata pale chini ambapo pana vyoo hakuna choo ambacho kinamjali mtu mwenye ulemavu. Kwa hivyo, ni vitu muhimu sana kuweza kutazama.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninamuunga mkono sana Mhe. Mohammed Said Dimwa, kwa maelezo yake ya hoja, lakini vile vile kwa maazimio yake yote ya hoja hii ambayo ameyatoa. Mhe. Mwenyekiti, sina mengi sana ya kuchangia lakini mimi naunga sana mkono hoja na wenzangu waichangie, ili kuona kwamba tunatenda haki kwa wenzetu wenye ulemavu, kwa sababu na sisi tuko nyuma yao katika kuelekea hilo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa ninamwita Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Hamza Hassan Juma ajitayarishe.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu, iliyoletwa na mheshimiwa makini kaka yangu Mhe. Mohammed Said Dimwa kwa kuwajali watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mara nyingi hupenda kunyanyuka na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe Mwenyekiti, vyama vingi vya siasa katika Ilani zao hazikuwasema watu wenye ulemavu. Lakini Chama cha Mapinduzi katika ukurasa wa 221 imewataja watu wenye ulemavu, kwa inavyowajali watu wenye ulemavu CCM na kuwathamini watu wenye ulemavu, hiyo ni kazi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Panya Ali Abdalla alisema hapa kwamba mzima wa leo ni mlemavu wa kesho, ni kweli. Mhe. Mwenyekiti, kilicho mbele yetu ni kuwajali watu wenye ulemavu, kuwathamini, kuwatendea haki na kuwasaidia pale ambapo wanahitaji misaada mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kuna siku moja nilikwenda pale Skuli ya Mtopepo nikamkuta mlemavu wa macho, yaani asiyeona jinsi vile alivyodhalilishwa na wale vijana pale mpaka akakaribia kugongana na gari, hata ile kumkamata mkono kumuondoa na kumuongoza njia walishindwa. Mhe. Mwenyekiti, nilisikitika sana na nililaani sana suala lile. Ikabidi mimi nishuke ndani ya gari nikawaeleza wale vijana.

Mhe. Mwenyekiti, watu wenye ulemavu wana haki ya kila kitu katika nchi hii, kwa sababu watu wenye ulemavu ni binadamu kama binadamu wengine. Mhe. Mwenyekiti, kilichobakia sasa ni kwamba kama alivyosema Mhe. Rashid Makame Shamsi kwamba hili sio jukumu la serikali peke yake, kwa sababu serikali ni watu na watu ndio sisi, kwa hivyo kila mmoja atimize wajibu wake ili kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu tunawathamini na tunawasaidia kwa misaada mbali mbali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis hapa alichangia na aliguswa, kwa sababu yeye anawawakilisha watu wenye ulemavu. Lakini na mimi nikaona sio vyema kumuachia Mhe. Mwantatu Mbaraka peke yake kwa sababu anawawakilisha watu wenye ulemavu, mimi leo ni mzima lakini kesho naweza nikatoka hapo tu nikapata ulemavu wa aina mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niunge mkono asilimia mia kwa mia ripoti hii na naunga mkono kuhakikisha kwamba tutahakikisha kwamba watu wenye ulemavu tunawathamini na tunawalinda, tunawatetea na kupata zile haki zao kama inavyopaswa. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuichangia hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa, kuhusu suala zima la utekelezaji wa haki za walemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi Mhe. Mohammed Said Dimwa alikuwa katika hoja yake anatukumbusha wajibu wetu. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika hoja ya Mhe. Mohammed Said Dimwa, hakuna sehemu aliyosema serikali itunge sheria, kwa sababu tayari serikali imeshatunga sheria, sera ipo, maazimio na mikataba ya kimataifa ipo lakini tuna tatizo katika utekelezaji wa sheria hizi. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyofahamu kwamba jukumu la kuendesha nchi amekabidhiwa Mhe. Rais aliyekuwepo madarakani, ikiwa wakati uliopita, wakati huu na wakati ujao. Kwa hivyo, kazi kubwa ya Mhe. Rais inakuwa kutekeleza zile sheria ambazo zilizotungwa na Baraza la Wawakilishi, na Baraza la Wawakilishi kazi yetu ni kuisimamia serikali kutekeleza yale yote ambayo yamo katika sheria.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais kwa mujibu wa Katiba yeye ndiye anayefanya kila kitu, lakini Katiba hiyo hiyo ndiyo imempa mamlaka kuteuwa wasaidizi wake, kuanzia Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Manaibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na wengine wote. Sasa kama hivi vyombo vyote vipo vimeteuliwa na sheria tayari tumetunga lakini bado haitekelezwi. Mimi nadhani hapa lazima tujiangalie upya.

Mhe. Mwenyekiti, suala la sheria katika suala zima la majengo tumetunga sisi na sheria imezungumza vizuri sana kwamba majengo yatakayojengwa yawe na miundombinu rafiki ya kutumika kwa ajili ya ndugu zetu wenye ulemavu. Lakini leo tujiulize, kuna majengo ya serikali, maana yake ukiwacha majengo ya watu binafsi, kwa sababu katika ile sheria inazungumzia majengo ya *public*, yaani majengo ya kutumiwa na jamii yawe na miundombinu rafiki. Lakini leo tunaendelea na mikataba mbali mbali ya kujenga ujenzi wa maskuli, vituo vya afya na mambo mengine lakini bado hatujaweza kuangalia miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa najaribu kuwakumbusha watendaji ambao waliokabidhiwa hizi dhamana, mimi nafikiri waangalie sheria zinasemaje, maazimio ya kimataifa yanasemaje ambayo Tanzania imeridhia ili kuweza kuhakikisha kwamba tunatekeleza kikamilifu, ili ndugu zetu wenye ulemavu waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuna lugha moja huwa sipendi sana kuisikia, kwamba tuwasaidie watu wenye ulemavu. Sio kuwasaidia tuwawezeshe. Maana yake Mhe. Mwenyekiti, kila siku mtu ukiwa unamsaidia unakuwa kama unamlemaza. Kwa hivyo, tuwawezesha, tuwape nyenzo au tuwape mbinu ili waweze kujitegemea maisha yao. Waswahili wanasema maisha yote mtegemea cha ndugu hufa maskini. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu pamoja na sisi wenyewe katika maeneo yetu mbali mbali tujitahidi kuwawezesha walemavu ili waweze kujitegemea wao wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia suala moja na kwa kuwa hiki ndio chombo muhimu sana katika nchi yetu, huu ni muhimili ni chombo cha kutunga sheria. Mimi nadhani ni lazima Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa leo uko wewe hapa basi salamu zetu hizi tunaomba umpelekee Mhe. Spika, kwamba hatuwezi tukawasema wenzetu wakati sisi wenyewe tuna kasoro. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nadhani umeshawahi kutembelea nchi ya China. China baada ya kupitisha sheria hizi au maazimio ya kimataifa kuhusu watu wenye ulemavu, basi hata yale majengo makongwe ambayo yalijengwa kwa muda mrefu uliopita basi yalifanyiwa miundombinu yakakarabatiwa ili walemavu waweze kuyatumia. Mimi mwenyewe katika ziara hiyo nilishiriki pamoja Mhe. Spika, mstaafu tulikwenda na tukaoneshwa majengo ambayo mwanzo yalijengwa yalikuwa yakitumia ngazi za kawaida za miguu. Lakini tukaambiwa kwamba kuna *lift* na tuliona sisi wenyewe tukapanda. Kwa hivyo, hata hili jengo letu la Baraza la Wawakilishi, mimi naamini kwamba wataalamu wetu, sasa hivi tunazungumzia kutafuta bajeti ya kurekebisha *echo* ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, nadhani sasa tutafute namna ya kutafuta uwezeshaji wa kuweza kutengeneza *lift*, na kwa bahati nzuri jengo letu lina ghorofa moja tu. Kwa hivyo tuweze kujenga *lift* ambayo wenzetu hawa wataweza kuitumia kwa ajili ya kuingia ndani ya jengo letu la Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema kwamba kwa kuwa sisi wenyewe tuna kasoro basi hata nguvu ya kuwasema wenzetu inakuwa ni ndogo. Kwa hivyo tuanzie sisi ndani ya Baraza la Wawakilishi na mimi Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ni mjumbe wa Kamati ya Uongozi na bahati nzuri Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) aliyeleta hoja hii na yeye mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati ya Uongozi kikao chote nitakachokaa cha Baraza la Wawakilishi tutaanza kujadili hoja ya kuweka *lift* ya kuingia ndani ya Baraza la Wawakilishi ili mtu yeyote aweze kuingia katika jengo hili.

Nataka nimalizie ili niokoe muda Mhe. Mwenyekiti, katika sera ya watu wenye ulemavu imeeleza wazi wazi kuwapa fursa watu wenye ulemavu leo Mhe. Mwenyekiti, tulilizungumza mpaka katika fursa za ajira katika Mawizara yetu mbali mbali mpaka leo Mhe. Mwenyekiti, sijaona *priority* katika masuala ya ajira na ajira kila siku zinatangazwa, lakini katika vile vigezo haijaonyeshwa hata pahala pamoja kwamba mtu mwenye ulemavu atapewa mazingatio maalum. Sasa hili nilikuwa naliomba Mhe. Mwenyekiti, katika ajira tunazoendelea kuzitangaza wamo watu wengi ambao wanajaza lakini wamo watu ambao wenye ulemavu. Kwa hivyo naomba sana miongoni mwa matangazo ya ajira basi suala la

*incentives* kwa watu wenye ulemavu lizingatiwe ili kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu tunawapa fursa ili waweze kujitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua katika maeneo yetu wamo watu wengi wenye ulemavu wanaishi na familia zao, wanaziongoza familia zao kwa sababu gani wamewezeshwa sio wamesaidiwa wamewezeshwa ndio maana wanaweza kuhudumia hizo familia zao. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika nchi za ulaya barabara nyingi ukiangalia zina maeneo zimewekwa *space* katika vile vikuta lakini vimevunjwa vimetengenezwa utaratibu ambao watu wanaweza wakapita hata na vile vigari vyao au vile vibaiskeli vyao, kama alivyosema Mhe. Amina Salum Ali na mimi niliwahi kuwa Waziri ambaye nilikuwa nashughulikia masuala ya watu wenye ulemavu. Kwa hivyo nimejaribu kupata elimu kubwa sana wenzetu kitu walichofanya kupitia makongamano na maazimio ya watu wenye ulemavu Serikali waliweza kufanya marekebisho katika maeneo mbali mbali kupita tu na ile *pressure group* ya watu wenye ulemavu. Kwa hivyo na sisi bado hatujachelewa kama walivyosema wenzangu kwamba kuna baadhi ya miundombinu tunayo nafasi ya kuifanyia marekebisho ili hao ndugu zetu wenye ulemavu wakaweza kuitumia vizuri.

La mwisho kabisa kabisa Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa inapokuja Miswada ninasoma kwa sababu ninaona. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tujiulize leo ndani ya Baraza la Wawakilishi tukija tukimpata mlemavu mwenye ulemavu wa macho, je kuna maandishi hapa, kuna chombo chochote cha kuweza kuandika maandishi ya wenye ulemavu. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, pia na hili naomba sana katika bajeti yetu ya Baraza la Wawakilishi tuandae utaratibu wa kutenga bajeti ya kutengeneza au ya kununua mashine ya kutengenezea yale maandishi ya *braille* ambayo wenzetu wenye ulemavu wa macho wataweza kutumia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naunga mkono hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohammed, lakini ajaribu vile vile kuangalia na yale mapendekezo ambayo niliyoyapendekeza yaingie baadhi yao ambayo watahisi yaingie katika yale maazimio ili tuweze kufuatilia katika utekelezaji wake. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono kwa asilimia mia moja hoja ya Mhe. Dimwa ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Hamza Hassaan sasa ninamuita Mhe. Mwanaasha Khamis akifuatiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Majenzi, Usafirishaji na Ujenzi.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja aliyoileta Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kuhusu miongozo inayohusu miundombinu, majengo na barabara kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana sana Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kwa kuona kuwa ipo haja ya kuleta ndani ya Baraza lako hili Tukufu maazimio ya kuhusiana na suala zima la miundombinu ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, siku ya watu wenye ulemavu ya Tarehe 3 Disemba, Duniani nilihudhuria pale katika yale maazimio, tumeshuhudia maadhimisho yale ya watu wenye ulemavu kwa kweli ipo haja Serikali kuangalia tena upya au kupitia au kutuletea Sheria ya Watu Wenye Ulemavu hapa Barazani ili tuweze kuifanyia kazi, kwa sababu sheria ile ina mapungufu mengi pamoja na kupitia sheria nyingi ambazo zizonaletwa. Kwa hivyo naomba Serikali watuletee ile Sheria ya Watu Wenye Ulemavu tuiangalie na tuipatie ufumbuzi kuhusiana na masuala mazima ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, mtoa hoja katika maazimio yake alisema hapa kuwa Serikali ipitie au ifanye ukaguzi katika majengo yanayojengwa, hili ni kweli wapitie kweli kweli katika ziara yangu ya kamati ya Ustawi wa Jamii tulipitia vyuo mbali mbali au skuli mbali mbali ambazo zimejengwa na Serikali zipo lakini hazina mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu, mpaka nimethubutu kuuliza katika Skuli ya Chwaka, tumeingia maeneo ya Maktaba niliuliza pale je, katika eneo hili hakuna watu wenye ulemavu, wamesema wapo na wanashindwa kupata huduma ya maktaba kule juu kwa sababu tu ya miundombinu iliyokuwepo pale. Kwa hivyo nasema hapa lazima Serikali ipitie majengo yote ambayo wameyajenga na si kwa yale yaliyojengwa.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tayari hapa tuliambiwa na Wizara ya Elimu kuna skuli karibu tisa zinataka kujengwa za ghorofa na tayari michoro imeshaanza na tayari ujenzi umeshaanza, tumepitia skuli moja ambayo inajengwa ya Kijitoupele/Pangawe kama sikosei, lakini pia nawaomba sana Serikali wapitie zile skuli za ghorofa ambazo zinajengwa kabla ya kumalizika yale majengo tuone watu wenye ulemavu nao wanapata fursa kama wenzao wengine.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamesema mengi lakini na mimi niseme kuwa ni kweli sisi tuliokuwemo humu mara nyingi watu wenye ulemavu katika maelezo yao wanasema sote ni walemavu watarajiwa, Mhe. Mwenyekiti, ni kweli huwezi kujua Mwenyezi Mungu kakuandikia nini, huwezi kujua utafikia wapi. Kwa hivyo tukitengeneza misingi hii hapa kwa kutengeneza majengo yetu basi tayari na sisi walemavu watarajia tayari tumeshajiwekea ile miundombinu. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Serikali ilichukue hili na maazimio yote ambayo ameyaleta Mhe. Dimwa wayafanyie kazi. Mhe. Hamza alizungumza hapa ndani ya Baraza hili la Wawakilishi tayari peke yake chombo cha kutunga Sheria bado hakuna ile miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Kwa hivyo kama Baraza pia nalo tukae pamoja tuone tunawasaidia vipi ili na wao haki zao wapatiwe hawa watu wenye ulemavu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalotaka kuliona kuwa alilolizungumza hapa Mhe. Dimwa katika maazimio yake hizi kanuni inawezekana hapa tukatunga sheria nyingi na tunazitunga lakini kanuni zinachukua muda mkubwa sana, kutungwa kanuni katika zile sheria tulizozipitisha. Kwa hivyo naiomba Serikali tutapopitisha sheria na tayari zipo basi zifuate ule utaratbu wa kutunga kanuni kwa sababu hatuwezi kuweka mambo yote ndani sheria, kanuni ndio itakayofanya kazi. Kwa hivyo tunaomba sana sheria zinazopitishwa zitungiwe kanuni kwa haraka ili tuweze kuzifanyia kazi na hawa watu wenye ulemavu wajisikie na wao ni miongoni mwa watu wa jamii inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa hayo machache naunga mkono hoja hii ya Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimba) kwa asilimia mia na natumaini maagizo yote ambayo yametolewa katika hoja yake hii Serikali wayafanyie kazi ili na watu wenye ulemavu wajisikie kama na wao ni sehemu ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti nakushukuru ahsante.*(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti.** Sasa namuita Mhe. Mohammed Ahmada Naibu Waziri wa Miudombinu na baadae mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Maudline Cyprus Castico.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha mchana huu kuipitia na kuijadili hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimbwa) Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mpendae.

Kama walivyotangulia wenzangu na alivyotangulia Mhe. Waziri anayekaimu Wizara yetu hii Mhe. Amina Salum Ali kwamba Serikali tumeona umuhimu wa hoja yake hii na kusema la kweli nimpongeze sana kwani hoja imekuja wakati muafaka na nina matuamini kwamba yale yaliyopendekezwa humu basi nasi kama Serikali tutayafanyia kazi kwa maslahi ya wananchi wetu wote na hasa watu wenye ulemavu. Sote tunajua kwamba Serikali yetu inawajali watu wenye ulemavu na ndio maana sasa katika ilani yetu ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi Ibara 135 mpaka 137 imeelezea kuhusu namna gani Chama cha Mapinduzi iwapo tutapata ridhaa ya wananchi tutawafanyia watu wenye ulemavu. Kwa hivyo nina imani kubwa sana Mhe. Mohammed Said Mohammed ali-*point* hoja hii kwa ajili ya kujua kwamba Chama cha Mapinduzi pia kinawajali watu wenye ulemavu na ndio maana ikawapa kipaumbele na kuwawekea ibara zile.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kuna masuala yamezungumzwa tofauti yanayohusiana na Wizara yetu ya Ujenzi hasa katika sekta ya majengo na vile vile barabara, usafiri ambao unatumiwa na wananchi hasa wa dala dala na gari za abiria nyengine. Ni kweli kwamba mpaka sasa hivi katika masuala ya majengo hatujakuwa na Kanuni wala Sheria lakini wataalamu wetu wameanza kwa kuweka muongozo ambao hadi hivi sasa unafanyiwa *review*.

Muongozo huu unaelezea kufikiwa na kupitika kwa watu wenye ulemavu kwenye majengo yetu, nashukuru katika kamati iliyoundwa pia wapo watu wanaotokana na ulemavu, na nina imani kubwa sana wadau tofauti walioshirikishwa katika kamati hii basi watakuja na jambo zuri zaidi ili baadae sasa yale mapungufu yote ambayo tumeyaona kupitia majengo yetu kama ulivyosema majengo mengi yalikuwa hayana *lift*, mengine *round* zake haziko kama alivyosema Mhe. Mwantatu, vile vile wembamba wake unasababisha hata kama anakuwa na kigari cha kumchukua Mheshimiwa  mwenye ulemavu inakuwa tabu. Kwa hivyo muongozo ule utakapokuja Serikalini tutaupitia lakini tutahakikisha kwamba tunaufanyia kazi kwa maslahi ya wananchi wetu wote. Kwa hivyo mimi nimshukuru sana Mhe. Mohammed Said Mohammed na nimwambie kwamba wakati wote utakapopata ile taarifa ya kamati ile, basi Serikali haitosita kulifanyia kazi ile taarifa ya kamati kwa ajili maslahi ya watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wamezungumzia kuhusu masuala ya barabara ni kweli kulikuwa na mapungufu hapo kabla lakini baada ya kuja ile sheria ya barabara kutokana na marekebisho yaliyofanyiwa 2012 tumepanua sasa, hifadhi ya barabara na imekuwa sasa hivi bara zote za *main road* na barabara nyengine za miji na Wilaya zinatakiwa hifadhi yake isipungue mita 15 kutoka pande zote mbili. Tumeanza kwa kujenga barabara hii ya Mwanakwerekwe Makaburini mpaka Fuoni na tumeanza kwa kuweka njia maalum za kupita walemavu na tutahakikisha kwamba kwa barabara zote nyengine tunazozijenga na hii ikiwemo barabara ya Bububu/Mkokotoni na nyenginezo, basi kuhakikisha kwamba tunaweka suala la walemavu na vile vile njia kwa walemavu zinatiliwa mkazo.

Lakini vile vile nichukue nafasi hii kwa kutoa tahadhari sana kwa madereva wenye daladala baadhi ya wakati hizi alama wanakuwa hawataki kuzifuata na vile vile baadhi ya wakati wanakuwa wanakwenda mwendo kasi katika zile sehemu ambazo kuna alama maalum tumeziweka, sheria yetu ya usalama barabarani ya 2003 No.7 imeelezea kila kitu kuhusu sheria hiyo. Vile vile imeelezea kwamba wale makondakta na madereva ambao wanawanyanyasa watu wenye ulemavu sheria ile imeweka adhabu zao ambazo tunawapa watu wale. Kwa hivyo mimi kupitia Baraza lako Tukufu niendelee kutoa onyo na kuwaomba

sana Jeshi letu la Polisi liendelee kusimamia sheria zetu hizi, ili kwa maslahi ya watu wetu, kwani sote tunajua sasa hivi ajali zimekuwa nyingi sana kutokana na madereva kutotii sheria na vile vile kutojali utu wa binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze tena Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kuleta hoja yake binafsi na nina imani kubwa sana Wajumbe wote wameunga mkono kwa sababu ya umuhimu wake na sisi Serikali tutaichukua na tutaifanyia kazi kwa maslahi ya wananchi wetu wote. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:**Ahsante Mhe. Mohammed Ahmada sasa mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto karibu sana.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Mwenyekiti kwa heshima na taadhima kwanza na mimi napenda nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kuweza kuwepo hapa na pia kuweza kuchangia suala hili. Mimi niungane kabisa na mtoa hoja na nimpongeze pia kwamba ametoa hoja kwa wakati unaofaa hasa tukiwa katika kipindi cha kutaka kuendeleza majengo mapya, kupanua mji wetu wa Zanzibar wa Unguja na Pemba. Majengo mapya mengi yanaanza kujengwa na *plan* ya taifa inaonyesha kabisa majengo mengi yatakuwa ni majengo yenye ghorofa na majengo yatakayokuwa na nafasi kubwa. Kwa hivyo suala hili nadhani halijachelewa na halikosewa wakati ambao limeletwa.

Lakini pia nichukue nafasi kuipongeza Serikali katika baadhi ya maeneo ambayo wameweza kuona kabla kuanza kujenga masuala ya maeneo ambayo walemavu wanakuwa wanapita na sehemu ambazo zimekuwa zikitumika. Mimi nikiwa kama ni mzazi ambaye nimebahatika kupata kuzaa lakini pia kutembelea wagonjwa katika maeneo mbali mbali niliona mfano mzuri katika Hospitali ya Mwembeladu. Mwembeladu ni hospitali ambayo ni ya wazazi bahati nzuri walijenga hiyo njia ambayo inasaidia wanawake wanakwenda kule kwa urahisi wakiwa katika maumivu ya uzazi, lakini pia na walemavu wanapata nafasi ya kuweza kupita mule katika sehemu nzuri ambayo naamini kabisa aliyepanga lile aliliangalia mapema.

Lakini ukiangalia pia katika maeneo mengi ambayo yanafanyika sasa hivi utaona wameanza kufanya hicho kitu ukiangalia kama kituo cha kulelea watoto Mazizini, kuna sehemu ambayo inaweza kusaidia watoto kuingia lakini nadhani bado ametukumbusha wakati mzuri na muafaka Mhe. Mohammes Said Mohammed kuona kwamba hata majengo yetu binafsi tuyafikirie hivyo, kuanza kujenga kuhakikisha kwamba tunakuwa na vibaraza ambavyo vinaweza kusaidia watoto walemavu wanaweza wakakaa wakacheza kwa sababu Zanzibar tuna watoto wengi walemavu lakini wanafichwa majumbani kutokana na miundo mbinu ya kuwa mzazi akitaka kumchukua mtoto kwenda naye pahala sio rahisi akenda naye na kwenda kucheza naye kwa sababu itabidi ambebe kila pahala anapokwenda.

Kwa hivyo suala zima la kuzingatia ni vizuri ikaonekana na nadhani litakwenda kuzingatiwa na tutayafanya, kama alivyokwisha sema Waziri akiwemo Wizara ya Biashara Mhe. Amina alivyosema kwamba hili ni suala ambalo lipo na lipo kwenye sera, bahati nzuri hata ushirikishwaji wa walemavu walivyopata kwenda kwenye michezo nchi za nje ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanaangalia mbinu za wenzetu zinakuwaje. Kwa hivyo napenda nisisitize tu kwamba na nyumba zetu binafsi tunazoanza kujenga madamu limezinduliwa hili tuanze kuzizingatia ni yale majengo tu ambayo tunayarithi kwa sababu ya dharura ambalo

linawezekana kuhamisha na kupelekwa afisi nyengine ikabidi muingie kwenye Ofisi pasipokuwa na utaratibu wa awali wa kuona labda watu wengi wanaweza wakatumia.

Kwa hivyo naendelea kusisitiza kusema kwamba tushirikiane wazazi tushirikiane watu binafsi tushirikiane katika maeneo mbali mbali, lakini pia hata kwenye vyombo vya usafiri ni vizuri hata kama hawana jinsi ya kuwaingiza walemavu wanaweza kuwa na vifaa ambavyo wanaweza kuviweka mtu akatumia halafu wanakichukua wanakihamisha kukipeleka mahali pengine, lakini pia tuweze kuendelea kwenye maeneo ambayo ni ya *public* ambayo yanahitaji huduma ya kwenda kujisaidia nayo pia yazingatiwe sana, hasa katika sehemu za maskuli nilikuwa nazungumza na Mhe. Waziri wa Elimu hapa anasema kwamba suala hilo atalifuatilia kwa kuwa sasa hivi kuna elimu mjumuiko katika maskuli, katika elimu mjumuisho inasaidia kuwafanya watoto ambao wamekuwa amepungukiwa uwezo wa kuwa na viungo kamili inakuwa ni rahisi kuwafundisha kwa wepesi zaidi.

Lakini hata yule Waziri aliyesema kwamba ni vizuri kuwe na maandishi ya *Braille* yakaanza kuandaliwa mapema hata maskuli yakaweza kuwekwa na tuendelee kuhamasisha mapema, tusingoje mpaka tatizo limefika ndio tuanze kuhangaika kufanya mambo kwenda kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, nisingependa kusema mengi isipokuwa nipende kusema tu wazo hili ni zuri tuendelee kushirikiana nalo na hata huko majumbani tunapotengeza nyumba za kujisaidia, nyumba za kwenda mabafuni, majikoni, koridoo ni vizuri sana tukahakikisha kwamba tunajenga nyumba hizo. Natoa wito huu kwa sababu sasa hivi mji mzima Zanzibar utakapokwenda kubadilishwa jambo hilo liangaliwe. Nashukuru kwamba Serikali katika baadhi ya maeneo ambayo wamepanga *plan* mahususi waweze kurekebisha na kama nilivyosema kwamba sasa hivi majengo mengine yanajengwa ya Serikali ambayo yanaweza yakapangishwa basi pale yatakapoweza kurekebishwa tutaendelea kufuatilia kuhakikisha kwamba inarekebishwa ipasavyo, nadhani Waziri anayehusika ametusikia na akiwa anafuatilia kupeleleza wanayotoa vibali vya majengo ni vizuri na wao pia wakafatilia mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba tunakamilisha masuala hayo.

Baada ya kusema hayo napenda niunge mkono hoja iliyoletwa kwa 100, ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri, sasa namwita Mhe. Mtoa hoja ili aweza kuja kufanya majumuisho. Mheshimiwa karibu sana.

**Mhe. Mohamed Said Mohamed:** Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana, niseme tu hoja yetu hii kwanza niwatambue wale ambao wamechangia moja kwa moja. Waliochangia moja kwa moja ni Waheshimiwa Wawakilishi tisa naomba niwataje kwa ruhusa yako.

1) Mhe. Mwantatu Khamis Mbarouk
2) Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
3) Mhe. Panya Ali Abdalla
4) Mhe. Rashid Makame Shamsi
5) Mhe. Suleiman Makame Ali
6) Mhe. Hamza Hassan Juma
7) Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
8) Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji
9) Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Waliochangia kwa maandishi ni kama hawa wafuatao:

10) Mhe. Shehe Hamad Mattar
11) Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo)
12) Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira)

Mhe. Mwenyekiti pamoja na kuwa tulizungumza na tumeweka maazimio yale lakini pamoja na kuona kuna mazungumzo mbali mbali nimesema basi tuongeze maazimia kama haya yafuatayo.

**Azimio la Kwanza:**

1) Kwa sababu Baraza la Wawakilishi haina miundombinu na ndiyo kioo pekee sasa Baraza la Wawakilishi liweke bajeti ijayo ili kuweka *lift* na kununua mashine ya *braille* ile yenye nukta nundu.

2) Jengine kuwekwe kipaumbele katika fursa za ajira kwa watu wenye ulemavu, upendeleo maalum kwa sababu wako ambao wamesoma vizuri lakini wanakosa nafasi kwa sababu hawajawekewa vipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwantatu amezungumza kwa hisia tofauti na hisia kubwa sana. Ameizungumzia vizuri sana Sheria Nam 9 ya mwaka 2006, lakini tuseme tunaiomba serikali kifungu cha 13 na cha 12 kiendelee kutiliwa mkazo ili tuone basi sheria hii imekuwa vizuri. Lakini vile vile tunamshukuru sana Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, yeye alisema maazimio yote ni mazuri na hayana matatizo na sisi tunamshukuru sana, kwa sababu amejua ugumu wetu na kila mtu ni mlemavu mtarajiwa, si mimi, si mwengine na yeyote alivyo, hata uzee Mhe. Mwenyekiti, ni ulemavu.

Mhe. Panya Ali Abdalla na yeye alizungumzia kuhusu elimu kwa walemavu, lakini vile vile kuwapatia watoto walemavu, wale watoto ambao wanafichwa sasa kuwapatia elimu. Hilo ndilo jambo la msingi na tuipongeze sana serikali yetu, kwa sababu inajitahidi sana kuweza kuwafichua na kuweza kuwapa watoto wetu elimu. Waheshimiwa viongozi sitoweza kutaja yote kwa pamoja lakini nitakwenda kwa haraka kwa sababu muda unaelekea si rafiki sana.

Mhe. Rashid Makame Shamsi, yeye alitoa pongezi tunazichukua lakini vile vile alitanabahisha katika majengo yetu siyo ya serikali tu, nataka nimwambie katika ukurasa wa 7 ya hotuba yangu nimetaja majengo ya binafsi kutilia mkazo hizi huduma zote ambazo zinaendelea.

Lakini vile vile Mhe. Suleiman Makame Ali wa Ziwani kwanza tukupongeze sana kwa kuweza kusimama Kanuni ya Chama cha Mapinduzi au Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaeleza haikuwacha kitu na vyote imevitaja mle na huo ndiyo umuhimu wa chama bora na chama dume. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumza mambo mengi sana na moja ya yale ambayo tuliyapatia maazimio kwake, alisema tunazungumzia *echo* katika Baraza hili lakini hatuzungumzii miundombinu iliyokuwa rafiki ya watu wenye ulemavu, tuanze kwanza kushughulikia hili kuliko hata la *echo*, kwa sababu hili ni muhimu zaidi, kuna siku tutashindwa hata kuingia ndani kama kutakuwa hakuna huduma rafiki sana. Pia alizungumzia huduma rafiki ambayo tayari tumeiweka katika fursa kwa walemavu iwe ni fursa ya pekee katika ajira nayo tumeiweka katika maazimio.

Mhe. Nasor Salim Ali (Aljazira) yeye alikwenda mbali zaidi alisema kama bado hatujapata pesa za kuweza kutenga kwenye bajeti na ngazi mbili zinaonekana kwenye nyumba ya jengo letu ambalo linapanda juu, kwa nini moja tusifanye *round* tukaweza kupitisha kwa walemavu. Mhe. Nasor Salim Ali hili suala lako ni muhimu na tumelifikisha. Mhe. Mwenyekiti, ulifikishe ombi hili kwa Mhe. Spika, ili kuona njia rahisi zinaweza zikafanyika.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na yeye vile vile amezungumza mambo mengi lakini vile vile amezungumza mambo ya *zebra cross*. Mimi nasema tutii sheria bila ya shuruti. Hili nalijibu sana na lile la Mhe. Mohammed Ahmada, kuwa amezungumzia katika Wizara yake sana, watu watii sheria bila ya shuruti kuona *zebra cross*. Lakini hata hivyo Mhe. Mohammed Ahmada nilikuwa nikimuomba *zebra cross* siku nyingi sana na watu wengi wanakufa bado hili hajalitekeleza. Nikuombe sana tushirikiane kwa hili, ndiyo mambo haya mwisho tunayaleta hapa. Tunashirikiane sana katika kufanya hivi ili tuone basi tumekwenda vizuri. Lakini vile vile kushirikiane na jeshi la Polisi kuangalia sheria zile za barabarani zinatekelezwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mtu wa mwisho lakini kwa umuhimu wake sana Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, tunampongeza sana kwa sababu yeye ndiye mwenye familia na ndiyo mwenye watoto, jamii inakutizama wewe. Lakini umeliona hili kuwa miundombinu ya Skuli siyo rafiki. Tumeona matangazo mbali mbali kuna mtoto anapelekwa kwenda chooni na mzee wake hawezi anasema arudi nyumbani.

Mhe. Waziri wa Elimu tukuombe sana katika majengo haya ambayo yanajengwa uzingatie watu wenye ulemavu kuwa na vyoo ambavyo vitaweza kufika bila ya tabu yoyote. Yale matangazo yanayoletwa hayaletwi tu kuwa matangazo tuyaone, lakini yanatufundisha mambo ambayo tunayoweza kuishi na familia lakini na jamii kwa jumla. Wote kwa pamoja niwashukuru sana.

Niseme tu wengi tunasali lakini adhana ni lazima isomwe kwa sababu tunakumbushana na hapa hatuji kuwa tunazungumza mambo haya kama tunataka mtu fulani afanye hivi. Tunazungumza hichi kitu ili kukumbushana pengine tunaweza kuwa tumesahau, tunaweza kuwa tunatunga Sheria lakini *implementation* yake ikawa ngumu, tunaweza kutunga sheria lakini vile vile Kanuni tukachelewa kuzitunga, sio kila kitu tu Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kasema kama tunaweza kukitunga kwenye sheria lazima tuwe na Kanuni ambazo zinaweza kutuongoza.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo basi niseme naomba kutoa hojia, lakini Baraza lako Tukufu yote maazimio haya tuliyoyaazimia yafikie mbele. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe sasa nitawahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Muhammed Said Muhammed (Dimwa) wanaokataa, waliokubali wameshinda. Ahsante. Katibu tunaendelea na hoja iliyopo.

**HOJA ZA WAJUMBE**

**Maombi ya Wananchi wa Kisakasaka Zanzibar Kuhusu Namna Wanavyoweza Kufaidika Kutokana na Machinjio ya Wanyama Yaliyopo Kwenye Maeneo Yao.**

**Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa):** Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Kisakasaka ambao orodha yao na majina yao yamesainiwa katika karatasi hii yenye zaidi ya wananchi 79 naomba kuleta maombi haya kwa mujibu wa Kanuni ya 27(1) fasiri ya (f) na fasiri (n) kanuni ya 30 fasiri ya 1 – 6 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012, Mada ya Maombi.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 30, Fasiri ya 3 ya Kanuni ya Kudumu ya Baraza la Wawakishi toleo la mwaka 2012 wananchi ambao majina yao na saini zao zimeambatanishwa sambamba na ombi hili. Wananchi hao wanamadai ya msingi ya kufanya ombi hili ambayo watawasilisha kwa niaba yao katika Baraza hili na mimi ninayawasilisha leo hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kijiji cha Kisakasaka kilichopo Wilaya ya Magharibi (B) hapa Zanzibar kimekuwa maarufu kutokana na kutumia kwa muda mrefu katika shughuli za uchinjaji wa nyama ya ng'ombe hasa kwa ajili ya mahitaji ya wananchi na taasisi zilizopo hapa Zanzibar. Wananchi wa Kijiji hicho cha Kisakasaka wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa katika shughuli hizo na uchinjaji wa ng'ombe ili kuhakikisha kuwa shughuli hizo zinaendelezwa kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli hizo za uchinjaji zimekuwa zinanufaisha wananchi wetu wa Zanzibar kutoka maeneo mbali mbali ya Zanzibar wanaojishughulish na shughuli hizo kama chanzo muhimu cha kujipatia rizki. Pamoja na shughuli hizo huwanufaisha wananchi mbali mbali wa Zanzibar jambo ambalo ni la faraja sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Wananchi wa Kisakasaka wanaamini kwamba wanaweza kuweka utaratibu ambao mbali ya kuendeleza maendeleo ya Zanzibar kama nchi pia watanufaika zaidi kijiji cha Kisakasaka na wananchi wa Kisakasaka. Utaratibu huwo utakaowekwa na hatimaye utawafanya wananchi hao wa kisakasaka kutoa ushirikiano mkubwa katika kuendeleza shughuli hii ya uchinjaji nyama katika maeneo hayo.

Utaratibu huwo wa kutoa Kipaumbele kwa maeneo na wananchi wa maeneo yayotumiwa katika shughuli za uzalishaji mali si utaratibu mpya nchini Tanzania. Umekuwa ukitumika baadhi ya maeneo na kuonekana kuleta tija kubwa katika kuendeleza shughuli za uzalishaji katika maeneo husika kwa mfano katika ununuzi wa mazao mblai mbali Tanzania Bara yakiwemo mahindi, mpunga, korosho na mazao mengine, wanunuzi wamekuwa wakitozwa ushuru wa kijiji, fedha ambayo hunufaisha vijiji husika.

Aidha katika suala la gesi kwa Mkoa wa Kusini Tanzania utaratibu umewekwa kwa ajili ya kunufaisha maeneo inapotoka gesi.

**Madhumuni:**
Mhe. Mwenyekiti, kutokana na maelezo hayo wananchi wa Kisakasaka madhumuni ya kuleta Ombi hili mbele ya Baraza la Wawakilishi ni kuitaka serikali hii tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa madhumuni ya kuendeleza shughuli za uchinjaji wa nyama na wananchi kujipatia rizki zao kuzingatia mambo yafuatayo:

1) Kuweka kiwango cha ushuru wa shilingi elfu moja kwa ng'ombe mmoja atakaechinjwa katika maeneo hayo na fedha hizo ziwe kwa ajili ya maendelezo ya kijiji cha Kisakasaka.

2) Fedha hizo zitumike katika miradi ya maendeleo yanayokusudiwa kwa ajili ya Kisakasaka ikiwemo uimarishaji wa barabara za ndani, taa za barabarani, miradi ya maji, uchimbaji wa visima vya maji na miradi mengine kama hiyo.

3) Mbali ya kuomba kutozwa kwa ushuru huu kwa ajili ya wananchi wa Kisakasaka. Wananchi wa Kisakasaka wanaiomba serikali kwa kutumia vyanzo vyake mbali mbali kuendelea na kuongeza jitihada za kuimarisha machinjio hayo ya Kisakasaka ili yawe katika hali nzuri na kuepusha watumiaji wa maeneo hayo na maradhi yanaweza kujitokeza endapo maeneo hayo hayatatunzwa vizuri.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kisakasaka nafanya maombi kuwasilisha ili basi serikali iweze kuyachukua na kuweza kuyatekeleza maombi hayo. Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mohamed Said Mohammed (Dimwa) kwa ombi lako hili ulililoliwakilisha. Naomba niwatanabaishe Wajumbe kwamba kwa mujibu wa Kanuni yetu ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016 kifungu Nam. 30 kifungu kidogo kinasema hivi:

> "Baada ya kutimiza Masharti ya Fasili ya 3(3) ya Kanuni hii, Mjumbe Muwasilishaji wa ombi hilo atataja kwa ufupi sababu za kutaka ombi hilo lisomwe au kwamba liwasilishwe mezani au lipelekwe kwenye Kamati ya Kudumu au Kamati Teule, au ombi linalohusika lichapishwe lakini hakutokuwepo mjadala wowote kuhusu ombi la namna hiyo".

Kwa hivyo mtuelewe hivyo hakutokuwa na mjadala wowote kuhusu ombi la namna hiyo. Lakini pia vile vile kifungu kidogo cha 5 kinasema hivi:

> "Spika ataelekeza kwamba maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Fasili ya (4) ya Kanuni hii yapelekwe kwa Waziri anayehusika, na Waziri huyo alete taarifa ndani ya siku 90 au muda mwengine atakaoutaja"

Mhe. Waziri anayehusika anatakiwa afanye hivyo la kama itaonekana hazitoshi aweze kuleta taarifa nyengine muda gani ataweza kuleta kwa mujibu wa Kanuni hii.

Kwa hivyo Waheshimiwa sasa kwa kuwa haijadiliwi naomba niwahoji wale ambao kuwa wanaokubaliana na hoja hii ombi hili pamoja na nyongeza ya maombi yaliyoongezwa juu yake wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

## TANGAZO

**Mhe. Mwenyekiti:** Kamati ya Uongozi inatangaziwa na Mhe. Spika anataka wakutane mnamo saa 10:00 za jioni kuna Kikao cha Dharura. Sijapata mabadiliko mengine kama kuna mabadiliko. Waheshimiwa hapa nanong'onezwa kwamba kuna mabadiliko kwa vile itakuwa muda huu tumemaliza muda mzuri. Kamati ya Uongozi ikutane sasa hivi mara baada ya kikao hichi.

Naomba niakhirishe Baraza hili hadi kesho saa 3:00 panapo majaaliwa.

*(Saa 6:36 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 15/12/2017 saa 3:00 za asubuhi)*